

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA NNE

Kikao cha Hamsini na Tatu - Tarehe 23 Agosti, 2011

(Mkutano Ulianaza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefanikiwa kuongea na mgonjwa tulyempeleka Dar es Salaam jana, wamemfanya huduma zinazostahili na anaendelea vizuri. Pia amepokea msiba wa mke wake kama jambo ambalo haliwezi kuzuilkia, kwa hiyo anasema anashukuru sana. Katibu.

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha, 2011/2012.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 470

Ujenzi wa Soko la Kisasa Njiapanda - Himo

MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA aliuliza:-

Imefahamika kuwa Serikali ina mpango wa kujenga soko la kisasa kwenye eneo la Njiapanda - Himo kuanzia kipindi cha mwaka wa fedha 2010/2011.

(a) Je, maandalizi ya ujenzi wa soko hilo umefikia hatua gani na ujenzi unatarajiwa kukamilika lini?

(b) Je, wafanyabiashara wadogo wadogo kwenye eneo la Njiapanda - Himo na maeneo jirani ambao wanaandamwa na mgambo kila mara watanufaika vipi na soko hilo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) aliibusi:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Augustino Lyatonga Mrema, Mbunge wa Vunjo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ina mpango wa kujenga soko la kisasa eneo la Njiapanda - Himo. Katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Halmashauri ilitenga shilingi 92,444,700 kuititia Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (*ASDP*). Taratibu za manunuzi zimefanyika ambapo Mzabuni *EDCAT Interventional (I) Co. Ltd.* alishinda zabuni na kuchaguliwa. Halmashauri katika Bajeti yake ya mwaka 2011/2012 imetenga jumla ya shilingi 20,000,000 kuendeleza ujenzi wa soko hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, soko hili ni kwa ajili ya mazao ya wakulima na wafanyabiashara wadogo wa mazao ya kilimo/mifugo. Kutakuwa na mpango wa kukusanya mazao ya wakulima na kuyatafutia soko la uhakika ili wakulima wapate bei nzuri ya mazao. Kazi ya kukusanya, kupanga madaraja na kuuza itafanywa na vikundi vya wakulima ambavyo vitakuwa vimejengewa uwezo. Nawashauri wananchi kujiunga na vyama vya ushirika vilivyopo ili kunufaika na utaratibu huu kikamilifu. (*Makofii*)

MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA: Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri aliyoatoa leo asubuhi. Sasa kwa kuwa Serikali pale Himo inafanya kazi, mnaanza kujenga hili Soko la Kimataifa ambalo litakuwa na manufaa makubwa kwa wananchi wa Vunjo na Mkoa wa Kilimanjaro, pili usambazaji wa maji, naona mtandao mzuri pale Himo unaenda vizuri, lakini tatizo kubwa ninaloliona pale Mheshimiwa Waziri ni kwamba kwa miaka 15 kuna shughuli nyngi haziendelei pale, miundombinu imeshindikana, viwanja vya kuchezea watoto wa shule kutokana na kwamba hakuna fidia iliyotolewa na kuna watu 342 wanadai fidia kwa zaidi ya miaka 15 na kwa ajili hiyo Mji ule haujengeki, hausongi mbele, haupigi hatua ingawa Serikali ina nia nzuri sana. Sasa swali ni kwamba Mheshimiwa sijui utafanyaje kutusaidia pale Himo ili Mji ule u-*generate* kama ilivyo kuwa lengo na madhumu ya Serikali?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Augustino Lyatonga Mrema, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa mimi nimpongeze sana Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema kwa kazi hii ambayo anaitetea na kuipigania pale. Waziri wa Afrika Mashariki aliposimama hapa, alizungumza kuhusu umuhimu wa kuona kwamba mazao yote tunayapeleka katika eneo moja badala ya kuitisha kwenye vichochoro na hivyo kuinyima Serikali mapato. (*Makofii*)

Aliposimama hapa Profesa Maghembe nae alisema jambo hilo hilo, sina haja ya kurudia. Kwa hiyo, jambo ambalo anali-*address* Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema ni jambo la msingi, la kisasa, huu ni mtindo wa kisasa katika kufanya mambo. Sasa kuhusu hili la mipango na kwamba mambo yamefanyaje, Mji ule wa Himo ni Mji Mdogo, Mamlaka ya Mji Mdogo na ukisema hii ni Mamlaka ya Mji Mdogo, maana yake *it is a planned area*, ni eneo ambalo huwezi kujijengea holela, lazima uoneshe nguzo za umeme zitapita wapi, useme mitaro ya maji itapita wapi. Ukihatamka hivyo tu, hapo maana yake hakuna ma-squatter tena, maelekezo na maagizo ambayo tumetoa katika Mamlaka hili maana yake kuna Mtendaji pale ni kwamba ahakkishe kwamba jambo hili linafanyika. Kinacholeta tatizo hapa ni hili ambalo tumejibu juzi hapa kwamba kuna kesi ambayo tumekwenda Mahakamani kusitisha na kusimamisha mpango mzima wa kupanga lile eneo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tumetoa maelekezo, yapo mawili, hatuwezi kufanya jambo lolote hapa mpaka kesi ile imalizike au wananchi wale waliokwenda Mahakamani waamue kuondoa kesi ile Mahakamani, wairudishe kwenye Halmashauri wazungumze. Yote mawili tumetoa maelekezo jana na leo asubuhi kwamba wafanye hivyo kwamba kama kesi ile ikiondolewa pale, mimi naahidi kwa niaba ya Serikali hapa na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tutafuatilia jambo hili ili fidia ile iweze kupatikana. (*Makofii*)

SPIKA: Kwa hiyo, kazi kwa Mbunge kuwaambia wale wakaiondoe.

MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa tatizo linalowakabili wananchi wa Tarime hasa Mji Mdogo wa Sirari linafanana kabisa na sawa kabisa na Njiapanda ya wananchi wa Himo, namuuliza Naibu Waziri, Serikali itajenga lini soko la kisasa katika Mji Mdogo wa Sirari ili wananchi wa Sirari wasipate matatizo ya kuuza mazao ya chakula na mazao mengine ya biashara kwenda Kenya kwa njia za panya?

SPIKA: Na nyie mko Mahakamani? Maana yake umesema sawa sawa kabisa, haya Mheshimiwa Waziri jibu nafikiri unaifahamu Miji yote hii. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkoo, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chacha Nyangwine, Mbunge wa Tarime, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hawa nadhani hawapo Mahakamani kama ulivyo sema, pale anaposema Sirari, mimi nimefika pale na nimepaona. *Issue* ya kujenga soko kama hili linalozungumzwa hapa ni *issue* ya Halmashauri yenyewe, kama Halmashauri ya Wilaya ya Tarime inafikiri kwamba kuna haja ya kuweka pale Soko la Kimataifa kama tunavyosema ambayo nakubaliana nae kwa sababu kimsingi Serikali inaona kwamba kuna umuhimu wa kufanya hivyo, haya mazao yana *slip slip* hivi, yanatoka huku, yanapita huku wala huna hakika kama *TRA* wanapata hizo hela, hata Halmashauri yenyewe kama inapata hizo hela. Kwa hiyo, ukiwa na mahali ambapo unaweza kuwekeza watu wote wakaenda pale, sisi tutapata mapato ya Serikali na kama tutapata mapato ya Serikali, mimi siwezi kusimama hapa kusema kwamba msifanye hivyo, lakini *the bottom line is lazima muipitishie katika Halmashauri*, Halmashauri iseme kwamba kwetu sisi hiki ni kipaumbele baada ya hapo sisi kama Serikali sasa tutasaidia katika mpango mzima. (*Makof*)

Na. 471

Tatizo la Maji - Maharaka, Sewe, Doma na Msongozi

MHE. AMOS G. MAKALLA aliuliza:-

Vijiji vya Maharaka, Sewe, Doma na Msongozi vipo jirani na Mbuga ya Wanyama ya Mikumi na vina matatizo ya maji:-

- (a) Je, Serikali kupitia *TANAPA* ina mpango gani wa kusaidia uchimbaji wa visima katika vijiji hivyo?
- (b) Je, utekelezaji wa kazi hiyo utaanza lini?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkoo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amos Makalla, Mbunge wa Mvomero, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vijiji cha Maharaka, Sewe, Doma na Msongozi ni miongozi mwa vijiji ambavyo vipo jirani na Hifadhi ya Taifa ya Mbuga za Wanyama ya Mikumi. Aidha, Kijiji cha Doma kimechimbwa kisima chenye uwezo wa kutoa maji lita 50,000 kwa saa kupitia Programu ya *RWSSP* ambapo kazi zinazoendelea ni uwekaji wa miundombinu ambapo zimetengwa shilingi milioni 350 katika mwaka wa fedha 2011/2012. Kijiji cha Msongozi kilichimbwa visima vifupi vitano na vinatoa maji ingawa hayatoshelezi mahitaji kutokana na ongezeko la idadi ya watu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Halmashauri imeshawasilisha makadirio ya uchimbaji wa kisima kirefu katika kijiji cha Mkata mwezi Machi, 2011 kwa gharama za shilingi milioni 24 kwenye Shirika la Hifadhi ya Mbuga ya Wanyama Tanzania (*TANAPA*) - Mikumi ili iweze kusaidia uchimbaji wa kisima katika kijiji hicho. *TANAPA* imeomba Halmashauri kuwasilisha andiko la mradi huo ili kutimiza azma hiyo.

Mheshimiwa Spika, mradi huu utaanza kutekelezwa mara baada ya Shirika la Hifadhi ya Wanyama Tanzania (*TANAPA*) itakapokubali kusaidia kupeleka huduma ya maji katika maeneo husika.

MHE. AMOS G. MAKALLA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza:-

Kwa kuwa katika majibu amegusia kijiji cha Doma na Msongozi kwamba maji hayatoshi, lakini hajaongelea vijiji vya Maharaka na Sewe. Je, miundombinu inayojengwa itafikia hivi vijiji vya Sewe, Maharaka na Msongozi?

Kwa kuwa *TANAPA* wanahitaji andiko toka Halmashauri wameshaporea maombi toka katika kijiji cha Mkata na kwa mawasiliano aliyonayo na *TANAPA*, je, andiko hilo likikamilika ndani ya wiki moja, *TANAPA* wanaweza kusaidia kijiji cha Mkata kupata mradi huu wa maji?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Amos Makalla, Mbunge wa Mvomero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa labda nieleze hapa kwamba ni nini kilichotokea. Kule anakotaja Mheshimiwa Makalla yupo *right* kabisa anachosema, lakini nataka nimwambie kitu kimoja, ukienda Doma pale walipoulizwa na *TANAPA* ninyi mnachotaka ni nini? Ni maji au mnataka nini? Wakasema tunataka Kituo cha Polisi, wakasema hivyo na Makalla anajua hiyo, wakasema tunataka Kituo cha Polisi. Na sisi katika *O and OD Opportunities and Obstacles to Development*, wananchi wakisema kwamba sisi tunachotaka ni hiki, hatuwezi kupuuza pamoja na kwamba Doma tumewapeleke maji pale, nilitaka kwanza tuelewane katika hilo. (*Makofii*)

Sasa hivi vijiji vingine anavyovisema hapa, anavyosema kwamba navyo havijaombewa, navyo tunesema kwamba vitaingizwa katika hayo maombi tunayoyazungumzia hapa na sisi wenyewe tutasaidia hata kama ni kuandika barua, tutasaidia kuandika barua kuhakikisha kwamba *TANAPA* wanasaidia. Haya ni maombi *TANAPA* hii ni *Tanzania National Parks* watasema wao kwa ajili ya kujenga ujirani mwema ninavyofahamu mimi kama Kiongozi wa Serikali hapa, najua kabisa kwamba wanao utaratibu wa kushirikiana. Kwa hiyo, sina matatizo kabisa na vile vijiji vingine vinavyozungumzwa hapa, lakini nataka nimfahamishe Mheshimiwa Makalla, Mvomero tumewapangia shilingi 689,000,000 yaani milioni 689 zimepangwa pale. Kwa hiyo, ni suala la *priorities*. Hili la Mkata na kwamba andiko litakuwa limeandikwa wiki moja na tena kama anataka sisi TAMISEMI tutasaidia kupeleka hayo maombi, yeche atuletee tu hilo andiko, sisi tutasaidiana ili tuhakikisha kwamba tunapeleka *TANAPA* na *TANAPA* tutazungumza nao kwa niaba ya Halmashauri. (*Makofii*)

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa kuna tatizo kubwa sana la vijiji vinavyoishi kando kando ya Hifadhi kutokana na kwamba vyanzo vya maji vyote viro ndani ya hifadhi, mfano kule Kisese vijiji vya Bugalabanya, Semu, Butili, Matale, Mwasengeri, vijiji hivi vyote vina tatizo kubwa sana la maji ya binadamu na kwa ajili ya mifugo. Je, Serikali inasema nini hasa kwa wananchi hawa wanaoishi kando kando ya hifadhi kuhakikisha kwamba inachimba malambo makubwa waweze kupata huduma ya maji kwa ajili ya binadamu na kwa ajili ya mifugo? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mpina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mimi wala sipati tatizo kumuelewa Mheshimiwa Mpina, hapa tuelewane kitu kimoja, ukitaka maji hapa hakikisha kwamba msitu hauguswi, ukitaka maji hapa, hakikisha kwamba watu wanapanda miti. Huhitaji kwenda Chuo Kikuu kuelewa kwamba ili maji yapatikane panda miti, *that is the bottom line*. Usipopanda miti patakuwa jangwa, wanyama watahama na watu watahama wataondoka pale, sasa ukishahifadhi pale unasema sasa tunataka chanzo hiki kitupatite malambo na huyu ni mfugaji anayezungumza hapa na mimi nimekwenda mpaka kwake Mheshimiwa Mpina tulikuwa nae hapa safari iliyopita.

Mheshimiwa Spika, sisi tunasema hapa, tutashirikiana nae katika kuhakikisha kwamba tunapata haya malambo, lakini lazima tu-*coordinate* haya mambo kwa sababu mkimsikiliza hapa Waziri wa Maliasili na Utalii anachozungumza ni kuhifadhi, sasa tunataka tuone jinsi ambavyo tunaweza tukaratibu mambo pale ili tusije tukaingiliana katika utaratibu mzima wa kupata haya

malambo anayosema, lakini sisi tutashirikiana nae ili kuhakikisha kwamba malambo hayo yanachimbwa, waweke tu kwenye programu yao. (*Makofi*)

SPIKA: Miti anayosema mpande, inayotunza maji, maana kuna miti mingine inakula maji yenye. (*Makofi*)

Na. 472

Tatizo la Maji katika Kata ya Nyakamwaga

MHE. LOLESEA J. M. BUKWIMBA aliuliza:-

Vijiji vya Nyakamwaga, Buyagu, Kasungamile, kashishi na Bufunda vilivyopo katika Kata ya Nyakamwaga, Wilaya ya Geita vina tatizo kubwa la upatikanaji wa maji.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta maji ili wananchi wa maeneo hayo waweze kupata maji safi na salama?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kata ya Nyakamwaga ina vijiji vitano ambavyo ni Nyakamwaga, Buyagu, Kasungamile, Kashishi na Bufunda kuptitia Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijiji (RWSSP), Halmashauri iliweka kipaumbele katika vijiji vya Katoro, Inyara, Luhuha, Izunya, Nyakagomba, Chigunga, Chankolo na Chikobe. Mkandarasi amepatikana na shughuli za uchimbaji zinatarajiji kuanza mara baada ya kukamilika kwa taratibu za kusaini mkataba wa kazi hiyo. Katika mwaka 2011/2012 Halmashauri imepanga kutumia shilingi bilioni 1.5 kuptitia uhisani wa Benki ya Dunia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kero za maji safi na salama vijiji zinatatuliwa kuptitia programu ya RWSSP. Kuptitia dhana ya ugatuaji wa madaraka kwa wananchi (*D by D*), wananchi wanahamasishwa na kujengewa uwezo kuchagua teknolojia inayowafaa kuhusu miradi ya maji. Hivyo nashauri Halmashauri pamoja na Waheshimiwa Wabunge kama sehemu ya Madiwani kuhakikisha utekelezaji wa programu hii unazingatia na kuweka kipaumbele vijiji ambavyo vina matatizo makubwa ya maji kwanza kuptitia fedha zinatolewa kila mwaka. (*Makofi*)

MHE. LOLESEA J. M. BUKWIMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumzia jinsi ambavyo Nyakamwaga wapo kwenye programu hii ya maji safi vijiji, na Nyakamwaga ni kati ya Kata ambazo katika Jimbo la Busanda zina kero sana ya maji na akinamama wengi wanahangaika sana, wanasaifiri umbali mrefu zaidi ya kilomita 10 kwa ajili ya kufuatilia maji na vilevile katika Kata hii kuna kituo cha afya ambacho pia hakina maji. Kwa hiyo, ningependa kujua Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba Kata hii inapata maji?

Mheshimiwa Spika, vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Naibu Waziri, vijiji vya Katoro, Nyakagomba, Chigunga ni kweli vipo katika mpango wa vijiji kumi ambavyo vinatakiwa kuletewa maji kuptitia mpango wa Benki ya Dunia. Lakini mradi huu kwa kweli umekuwa ni muda mrefu sana na wananchi kwa kweli wamekosa imani kwa sababu hata mwaka jana pia katika Bajeti kulionyesha kabisa kwamba wataweza kuhudumiwa maji, lakini hakuna kilichoendelea. Kwa hiyo, ningependa kujibu pia kwamba ni lini sasa mradi huu utaweza kuanza rasmi? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba niseme tu kwamba ile Kata ya Nyakamwaga haipo kwenye programu. Lakini haina maana kwamba programu

haitawenza kupeleka maji pale, ni kwamba Halmashauri ya Wilaya inabidi iweke kama kipaumbele katika awamu ya pili ambayo inaanza mwezi wa saba. Kwa hiyo, naomba sana Halmashauri husika iweke vijiji vya Nyakamwaga katika awamu ya pili. (*Makofii*)

Sehemu (b) naomba nikiri kweli kumekuwa na ucheleweshaji wa utekelezaji wa mradi wa vijiji kumi. Lakini tumeshajua sababu na tutazielezea tutakapokuwa tuna-*wind up* Bajeti yetu jioni. Sababu ambazo zimesababisha zimesababisha tukafikia pale na Serikali imejipanga vipi kurekebisha hali hiyo na hasa katika awamu ya pili. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante, ambayo inaanza mwezi wa saba, mwaka gani? Hiyo awamu ya pili Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Awamu ya pili inaanza mwezi Julai, 2012.

SPIKA: Aah *okay!* Ahsante, tunaendelea na swalii.

MHE. SUSAN L. A. KIWANGA: Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kuwa matatizo ya maji katika Mji Mdogo wa Ifakara ni makubwa sana takribani wananchi 70,000 wapo kwenye huo Mji Mdogo na mradi mkubwa unaoanza Mto Lumemo - Kiburubuto umesimama mpaka hivi sasa na kwenye Bajeti nimeona wametenga shilingi milioni 500 tu ambapo haitafaa kwa chochote. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi wa Mji Mdogo wa Ifakara wapate maji takribani wanatakiwa wapate lita milioni 2.5 kwa siku na sasa hivi wanatumia visima sita tu vyenye lita 600,000 kwa siku?

SPIKA: Mheshimiwa Susan, yaani ni swalii jipya kabisa kabisa. Naomba atajibu Waziri wa Maji, atakapokuwa anajibu maana ni jipya kabisa. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. (*Makofii*)

Na. 473

Ukamilishaji wa ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam - Mingoyo

MHE. SELEMANI S. BUNGARA aliuliza:-

Katika zoezi la kukamilisha ujenzi wa barabara ya kutoka Dar es Salaam - Mingoyo, wananchi wa vijiji vya Kiwawa, Hotelitatu, Mandawa, Mirumba, Mtandi, Kiranjeranje na Mbwemkuru wamebomolewa nyumba zao kupisha ujenzi wa barabara hiyo:

Je, ni lini Serikali itakamilisha malipo ya fidia kwa wananchi ambaa bado hawajalipwa fidia zao?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Selemani Saidi Bungara, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekwishakamilisha malipo ya fidia kwa wananchi ambaa walistahili kulipwa kwa mujibu wa sheria. Mwaka 2005 jumla ya shilingi 131,242,495.00 zililipwa kwa wananchi wa vijiji vya Kiwawa, Hotelitatu, Mandawa, Mirumba, Mtandi, Kiranjeranje na Mbwemkuru.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2008, baada ya miaka mitatu kupita Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa iliwasilisha madai mengine ya watu 52 wa kijiji cha Kiranjeranje yenye jumla ya shilingi 154,578,000.00. Ili kujiridhisha na uhalali wa madai hayo, Ofisi ya Wakala wa Barabara ikishirikiana na uongozi wa Mkoa wa Lindi na Wilaya ya Kilwa ilifanya tena tathmini na kubaini kuwa ni wananchi 21 tu ndio walostahili kulipwa fidia katika kijiji cha Kiranjeranje. Wananchi hao walilipwa jumla ya shilingi 86,770,000.00 mwaka 2010. (*Makofii*)

MHE. SELEMANI S. BUNGARA: Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imethibitisha imekamilisha malipo hayo, je, naweza kupata majina ya walilipwa na fedha walizolipwa? Swali la kwanza.

Swali la pili, je, kuna wananchi ambao wanadai mpaka sasa hivi hawajalipwa, je, Mheshimiwa Waziri utakubaliana na mimi kwenda Kilwa tukakutane nao ili tutoe utata huu kwa kuwa hawajalipwa?

SPIKA: Ahsante kwa kuuliza kwa kifupi. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, suala la kupata majina si gumu, tutampatia. Lakini baada ya kipindi cha maswali atuone, tutaweza kujadiliana. Lakini napenda nimhakikishie tu kwamba mwaka 2005 vijiji vyake vyote saba wananchi walilipwa fidia, kijiji cha Kiwawa, Hotelilatu, Mandawa, Mirumba, Mtandi, Kiranjeranje na Mbwemkuru vyote vililipwa jumla ya shilingi milioni 131,242,465. Lakini kama nilivyosema kwenye swali, jibu langu la msingi kwamba mwaka jana ndiyo tulilipa wengine wa ziada 21. La pili, angependa tufuatane naye nikawahakikishie wanakijji, mimi nadhani nikishampa ile orodha kama anaona hairidhishi basi bado sisi tupo tayari wakati wowote kufuatana naye kuwaeleza wananchi kwamba tayari tumeshawalipa fidia yao.

MHE. MURTAZA A. MANGUNGU: Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika, ningependa kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba eneo la Njia Nne, Mingumbi, Chumo, Kipatimo wananchi walivunjiwa nyumba zao na walipoteza mali zao hawakulipwa fidia, hali ya kuwa walikuwepo pale kabla ya sheria ambayo inatamkwa kuwepo kwamba wamekuwepo tangu miaka ya 1905 mpaka 1920. Je, Serikali inatamka nini kwa wananchi hawa?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwa wananchi katika baadhi ya maeneo waliyosema ya Njia Nne, Kipatimo na kuendelea kwamba hawakulipwa fidia yao, naomba tu pengine kwa faida ya Waheshimiwa Wabunge kwamba Wizara ya Ujenzi inawalipa wananchi wale ambao wameguswa na barabara kwa kufuatwa na barabara. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Wizara au Serikali haiwezi kuonea wananchi, ningependa tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Ibara ya 13(6)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inazuia na inakataza sheria au utekelezaji wa sheria yoyote ambayo inaharamisha kitu kilichokuwa halali jana, kwa maana ya kwamba Sheria ya mwaka 2007 ilipopitishwa ambayo ilikuwa inaongeza wigo wa barabara mpaka mita 30 haikuhamisha wale waliojenga kati ya mita 22 na nusu mpaka mita 30 wote wanalipwa fidia. (*Makof*)

Ningemwomba Mheshimiwa Mbunge kama kuna Watanzania ambao wana hoja ya msingi kwamba walifuatwa na barabara nje ya mita ya 22 na nusu na hawajalipwa mpaka leo namwomba atufuate tuweze kulirekebisha suala hilo. Kwa sababu suala ni halali wananchi walipwe fidia yao. (*Makof*)

Na. 474

Ujenzi wa Barabara ya Mbeya – Chunya – Makongorosi

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA aliuliza:-

Ujenzi wa barabara ya Mbeya – Chunya - Makongorosi kwa kiwango cha lami na wakandarasi wawili wa kipande cha Mbeya - Lwanilo na Lwanjilo - Chunya wameshaanza kazi:-

(a) Je, Mkandarasi wa kipande cha Chunya - Makondorosi atapatikana lini?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza barabara hiyo toka Makongorosi mpaka Rungwa?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, usanifu wa kina wa barabara ya Mbeya - Chunya - Makongorosi yenye urefu wa kilomita 115 umeshamilika. Kazi za ujenzi zinaendelea kwa sehemu za Mbeya - Lwanjilo (kilomita 36) na Lwanjilo - Chunya (kilomita 36). Sehemu iliyobaki ya Chunya - Makongorosi (kilomita 43) Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali hivi sasa inaendelea na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara ya Makongorosi - Rungwa - Itigi hadi Mkiwa yenye urefu wa kilomita 413 kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami, kazi ya upembuzi yakinifu imekamilika. Aidha, usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni upo kwenye hatua za mwisho. Mara kazi hizo zitakapokamilika Serikali itaanza kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii. (*Makofii*)

MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA: Nakushukuru Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Unajua kwamba *charity* inaanza nyumbani na hii barabara ya Mbeya - Chunya - Makongorosi kuelekea hadi Rungwa ina umuhimu sana katika historia ya nchi hii pia katika ustawi wa nchi hii kwa kuunganisha Mikoa ya Kanda ya Ziwa na Mikoa ya Kusini. Mwaka 2008/2009, 2010 barabara hii ilikuwa inatengewa shilingi bilioni 10 kila mwaka, lakini mwaka huu imetengewa shilingi bilioni tano pamoja na kwamba Mheshimiwa Naibu Waziri ni pacha wangu. Mheshimiwa ni size yangu kabisa wametenga shilingi bilioni tano, sasa naomba wanahakikishie kwamba mwaka kesho barabara hii itatengewa zaidi ya shilingi bilioni 10, la kwanza.

Swali la pili, nawaomba hawa hawa ndugu zangu Mawaziri, ndugu zangu wawahakikishie wananchi wa Chunya kwamba barabara hii itaisha kabla ya llani ya Uchaguzi ya CCM ilioiandika ya mwaka 2014/2015 haijaisha? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mwambalaswa kwa kupigania sana ujenzi wa barabara ya Mbeya - Lwanjilo - Chunya - Makongorosi mpaka Rungwa na kuendelea. Naelwa barabara hii itafungua fursa za uchumi za Chunya Wilaya ambayo ni kupita Wilaya zote kuchanganya na Mkoa wa Mbeya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie kwanza Mheshimiwa Mbunge kwamba azma ya Wizara au Serikali kwa ujumla ni kuhakikisha kwamba tunaunganisha Makao Makuu ya Mikoa yote kufikia mwaka 2017. Ndiyo maana lazima barabara hii tuhakikishe inajengwa na kukamilishwa ili kutimiza hiyo azma ya Serikali. Kukamilishwa kwa barabara ya Mbeya - Chunya - Makongorosi - Rungwa - Itigi - Mkiwa ni kuunganisha Makao Makuu ya Mkoa wa Singida na Mkoa wa Mbeya na ndiyo maana tumeshaanza kuhanganya vile vile kuanzia Tabora kuja Sikunge mpaka Ipole. Maana kutoka Ipole ndiyo tuna-*branch off* kwenda Rungwa ili iende Mbeya kuunganisha Mkoa wa Tabora na Mbeya moja kwa moja na vile vile na ku-*branch off* kwenda Koga kwenda Mpanda ili tuungane na Tabora iungane moja kwa moja na Mkoa wa Rukwa. Lakini suala la pili naomba nimhakikishie Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa kwamba kutokana na azma hii ya Serikali tutatenga fedha zaidi na wananchi wa Chunya mkae tu mkao wa kula kwamba katika miaka michache ijayo barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami. (*Makofii*)

MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA: Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kuniona. Mheshimiwa Spika, kipande hiki cha barabara ya Mbeya - Lwanjilo kilianza tangu mwaka 2008 pamoja na kwamba mkandarasi aliyeuwepo hakulewana vizuri na *TANROADS* kutokana na malipo. Lakini tukumbuke kwamba hii ni barabara muhimu kama alivyokwisha kuzungumza Mheshimiwa Mwambalaswa. Nilikuwa nataka Naibu Waziri atuhakikishie kipande hiki cha barabara ya Mbeya - Lwanjilo kitaanza lini hasa kuwekwa lami. Maana nilikuwa huko siku za hivi karibuni mpaka nikapata pancha mara tatu mimi mwenyewe. Nashukuru sana. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza kwa ruhusa yako naomba nimpe pole kwa kupata pancha. Hii ni kawaida wakati barabara inajengwa kuwepo na mawe madogo madogo ya kuingia kwenye matairi. Lakini la pili napenda nimueleweshe Mheshimiwa Mbunge

kama alivyosema, barabara hiyo ya Mbeya - Lwanjilo ilipata matatizo na mkandarasi wa kwanza aliyejukwepo. Kazi ilisimama, akatupeleka huko kwenye ma-libitration baadaye Serikali ikaamua kumteua mkandarasi mwingine na kazi imeshaanza. Lakini ye ye mwenyewe anaweza kukubali.

Mheshimiwa Spika, nazi ya udongo (*earth work*) kwa barabara ya Mbeya - Lwanjilo ni kubwa kupita kiasi kupita milima na ndiyo maana mmeona udongo mwingi unachimbwa na barabara hiyo ukienda saa hizi unafikiri kwamba utaingia kwenye mashimo lakini yote ni kwa ajili ya kuhakikisha tunapata barabara ya kudumu, kilomita 36 siyo nyingi. Napenda kumhakikishia Mbunge kwamba tunajenga hiyo barabara na tutaikamilisha katika muda usiopita kipindi hiki cha llani cha Uchaguzi. (*Makofii*)

Na. 475

Tatizo la Walimu Kukosa Mishahara

MHE. SADIFA JUMA KHAMIS aliuliza:-

Serikali inatambua kuwa mpaka sasa wapo walimu ambao hawajapata mishahara yao kwa muda mrefu na tatizo hilo bado halijapatiwa ufumbuzi:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza ni sababu gani za msingi zilizopelekea walimu hao kutopata mishahara yao?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo hili?

NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sadifa Juma Khamis, Mbunge wa Donge, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tatizo la walimu kutolipwa au kucheleweshwa mishahara yao linatokana na sababu mbalimbali zikiwemo kushughulikia malipo ya mishahara ya walimu Makao Makuu ya Wizara kabla ya ugatuaji ambalo ugatuaji ulifanywa tarehe 1 Julai, 2009. Pili, walimu kuchelewa kuripoti katika vituo vyao walivyopangiwa au kuripoti katika vituo ambavyo hawakupangiwa awali na hivyo kusababisha ucheleweshaji wa kutuma taarifa za waajirwa wapya Hazina na tatu, baadhi ya walimu kutokamilisha taratibu zao za kiutumishi kwa wakati na hivyo kuchelewesha maandalizi ya malipo ya mishahara yao. Napenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali inaimarisha usimamizi na uendeshaji wa shule kwa kuwapatia mafunzo watendaji ya Halmashauri ili waweze kumudu vema majukumu yao.

Aidha, walimu wanahimizwa na kukumbushwa juu ya kutekeleza vema wajibu wao ikiwa na pamoja na kuzingatia taratibu za kiutumishi na kuripoti katika vituo walivyopangiwa kwa wakati, wakiwa na kumbukumbu sahihi na muhimu zinazowezesha Hazina na Idara Kuu ya Utumishi kuwaandalia mishahara yao mapema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa walimu ambao wameripoti katika vituo walivyopangiwa na hawajapata mishahara yao kuwasiliana na Halmashauri husika ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa. (*Makofii*)

SPIKA: Umeridhika? Mheshimiwa Mlata swali lingine la nyongeza.

MHE. MARTHA M. MLATA: Ahsante Mheshimiwa Spika, mimi napenda kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba kwanza kwa swali hili linaonekana ni swali ambalo lilitakiwa lijibiwe na TAMISEMI. Je, kwa ugatuaji wa masuala haya ya elimu kwenda TAMISEMI hawaoni kwamba wanawachanganya wananchi?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, lengo la ugatuaji wa madaraka kwenda kwa wananchi ni kuhakikisha kwamba tunawahudumia walimu kwa ufanisi na kwa ukaribu zaidi kuliko ilivyokuwa Wizara ya Elimu na atakubaliana na mimi kwamba sasa hivi kero nyingi sana za walimu zinapungua ukilinganisha na ilivyokuwa mwanzo. (*Makofi*)

MHE. MOESA J. MACHALI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa wakati nikichangia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu nililiza swali hapa kuhusiana na matatizo ya walimu kutokupandishwa madaraja yao katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu na kupitia Waziri wa Utumishi mama yangu Hawa Ghasia, aliahidi kuweza kufuatilia tatizo hilo kwa sababu kama vile kuna tatizo. Lakini mpaka leo hakuna kitu ambacho kimefanyika. Naomba kauli ya Serikali juu ya matatizo hayo kwa sababu walimu wanaendelea kulalamika mpaka leo hii? Ahsante sana. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, kwa kawaida huwa tunawapandisha vyeo walimu mara tu baada ya Bajeti. Kwa upande wa walimu wa sekondari mwaka jana wakati tuliviyowahamishia katika Serikali za Mitaa baadhi yao walishindwa kurekebishiwa mishahara au kupandishwa madaraja kwa sababu mafaili yao yalikuwa bado hayajafika katika Halimashauri. Kwa hiyo, mwaka huu katika watu ambao watapandishwa kwa idadi kubwa sana ni walimu wa sekondari pamoja na walimu wa shule za msingi. Kwa hiyo, bado tunaendelea kufuatilia. (*Makofi*)

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Ahsante Mheshimiwa Spika, napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa walimu wengi wamekuwa wakihangaika na kukopa kwa kufuatilia mishahara yao, je, Waziri atanihakikishiaje walimu hao wanapata mishahara kwa wakati muafaka na sehemu za vituo vyao vya kazi? (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, kama Naibu Waziri wa Elimu aliviyotangulia kusema sasa hivi hata juzi tulivyokutana na Chama cha Walimu suala la mwalimu kuchelewa kupata mshahara sasa hivi imeanza kuwa siyo kero. Tatizo ni pale ambapo mwalimu anaenda kuripoti kituo tofauti na alichopangiwa, na pale ambapo anachelewa kwenda kuripoti. Lakini wale ambao wanaenda kuripoti kwenye vituo vyao walivypangiwa na kwa wakati wanapata mishahara yao kwa wakati. Kama wapo wachache basi tuwasiliane. (*Makofi*)

Na. 476

Hujuma katika Usambazaji wa Vocha za Pembejeo

MHE. CONCHESTA L. RWEMLAZA aliuliza:-

Kumekuwepo na hujuma kubwa katika usambazaji wa Vocha za Pembejeo iliyogundulika kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Chato, unaohusisha Vijiji vya Muranda, Katende, Chabulonga, Muungano, Ilemela, Bupandwa, Mpuli, Nyakato, Katete na Busaka:-

Je, Serikali imechukua hatua gani kukabiliana na hujuma hizo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2010/2011 Wizara ilitoa jumla ya vocha 79,788 za mahindi, vocha 26,596 za mbolea ya kupandia na vocha 26,596 mbolea ya kukuzia zenye thamani ya Sh. 1,542,480,000/= kwa wakulima wa Wilaya ya Chato.

Mheshimiwa Spika, tathmini iliyofanywa na Wizara yangu kwa kushirikiana na Kamati ya pembejeo ya Wilaya ya Chato ilibaini kuwepo kwa ubadhirifu katika utoaji wa pembejeo yenyruzuki uliofanywa kwa kughushi saini, kuiba pembejeo na kujipatia fedha kwa udanganyifu. Watuhumiwa katika ubadhirifu huo ni pamoja na Maafisa Kilimo watatu ngazi ya Wilaya akiwemo Afisa Kilimo na Mifugo wa Wilaya (*DALDO*), Watendaji wa Vijiji 29, Wenyeviti wa Vijiji 11 na Mawakala sita.

Mheshimiwa Spika, ni kweli ni jambo la kusikitisha kwa sababu Watendaji hawa ndio walioaminiwa kusimamia zoezi la usambazaji wa mbolea katika maeneo yao. Hadi sasa hatua iliyochukuliwa na Serikali ni kuwafungulia mashitaka Polisi ambapo baadhi yao wamekwishafikishwa Mahakamani wakati upetelezi unaendelea. Aidha, Jeshi la Polisi linaendelea kuwatafuta Watendaji wa Vijiji na Mawakala walitoroka ili wafikishwe katika mkono wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuchunguza kwa umakini sakata la ubadhirifu uliotokea katika utoaji wa mbolea ili kubaini watu wengine waliohusika pamoja na kiwango cha ubadhirifu uliofanyika. Ili kubaini wabadhirifu hao na mbinu wanazotumia, Serikali imemwagiza Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalum (*Special Audit*) katika maeneo mbalimbali ambapo mbolea yenyruzuki ilitolewa. Matokeo ya ukaguzi yatatusaidia kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria wote watakaobainika kuhusika na hujuma katika mbolea kulingana na makosa yao. Aidha, taarifa ya ukaguzi itasaidia Serikali kuitambua mianya ya ubadhirifu ili kuiziba na pengine kurekebisha mfumo mzima wa utoaji wa mbolea zenye ruzuku.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, ubadhirifu wa ruzuku ya mbolea katika Wilaya ya Chato ulitambulika mapema, na katika barua ya Mkurugenzi yenyuze Kumbukumbu Namba *CDC/04/12/24* ya tarehe 8 Aprili, 2011 ambayo Mkurugenzi wa Halmashauri ya Chato alimwandikia Mkuu wa Wilaya, ambapo Mkuu wa Wilaya ndiye alikuwa Mwenyekiti wa kusaini vocha kwa mara ya mwisho ili malipo yatolewe kwa mawakala, alimtahadharisha kwamba, kuna udhaifu kwa kuchambua vocha ambazo zilikuwa zinakuja Wilayani: Je, ni kweli kama Maafisa Kilimo wamekamatwa, inakuwaje sasa Mwenyekiti wa pembejeo ambaye ndiye alikuwa anasaini, Mkuu wa Wilaya, kwa mara ya mwisho, hakuperekwa Mahakamani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kitendo cha Mkuu wa Wilaya kutokukamatwa kama Mwidhinishaji Mkuu, na kukamata watu walio chini yake, haionyeshi ubaguzi katika utekelezaji wa Sheria? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya kwa nafasi yake, ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya pembejeo katika Wilaya. Nafasi hizo zipo zinapanda juu. Mkoani yupo Mkuu wa Mkoa na kwenda juu, ni Waziri. Sasa kama Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya aliidhinisha na Watendaji wengine wakakiuka, maana yake inawezekana ukaidhinisha, lakini Watendaji wakakiuka. Lakini kama nilivyosema, zoezi zima linafanyiwa ukaguzi, na tunakagua, tunafanya *Special Audit* ambayo inakagua mfumo mzima. Siyo kwamba tunaangalia pale Wilayani tu, tunaangalia kutoka kwenye Vijiji, kwenye Kata, Wilayani, Mkoani, mpaka huko Wizarani ili kubaini ni nani hasa aliyehusika na kwa nafasi yake. Kwa hiyo, siyo kwamba wale walioamatwa ndiyo mwisho. Ndiyo maana CAG anakwenda sasa kukagua. Kama wengine tutawabaini, kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi, tutawachukulia hatua bila kujali nyadhifa zao. Lakini ni lazima tujiridhishe kwamba, wao ndio wamehusika.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyyoyatoa. Lakini napenda kujibu swali la nyongeza, linalohusu Mkuu wa Wilaya ya Chato, kuhusika au kutohusika katika tuhuma hizi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, tulipokea taarifa juu ya ubadhirifu uliotokea katika shughuli za usambazaji vocha za pembejeo Wilayani Chato. Tulimwagiza Mkuu wa Mkoa kuunda timu ya kufanya uchunguzi, wamefanya hivyo kwa kushirikiana na vyombo vya dola. Wale waliofikishwa Mahakamani ndio walioonekana kuhusika moja kwa moja na

hapakuwepo na ushahidi wowote wa kumfikisha Mahakamani Mkoo wa Wilaya, kwa sababu vyombo nya dola vilivyochunguza havikumwona Mkoo wa Wilaya anahuksika, ndio maana hakufikisha Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali hii inaheshimu sana Utawala wa Sheria, haimbagui mtu. Kama Mkoo wa Wilaya angekuwa amehusika na yeye angekuwa amefikisha Mahakamani.

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri, amesema wanafanya uchunguzi wa mfumo mzima, na kwa kuwa juzi hapa katika Mkutano wa Wadau wa Pamba, Mheshimiwa Waziri alitoa *offer* kwa *Cotton Development Fund* kwamba pesa takriban Shilingi billioni nane atazipitishia kwa mfuko huo ambao hauwezi hata kukaguliwa: Je, Waziri hayuko tayari kuhakikisha kwamba anangojea asitoe hiyo *offer* sasa mpaka tumeangalia mfumo mzima wa mambo haya ya vocha ili kuzuia upotevu wa fedha nyngi zaidi ya Serikali?

WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA: Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Kikao cha Wadau kilipendekeza kwamba fedha za pembejeo zipitie kwenye mfuko huo alioutaja. Lakini halii ilivyo ni kwamba, Kamati ambayo ilifanya uchunguzi na kuangalia matumizi ya pembejeo katika mwaka 2009/2010 ilionyesha kwamba, utaratibu uliofuatwa mwaka ule haukuwa mzuri, lakini ikaonyesha kwamba ni vizuri Bodi ya Pamba na Wakuu wa Wilaya ndio washirikiane katika kuchagua Mawakala na katika kuitisha ruzuku ya pembejeo ili kuhakikisha kwamba, fedha hizi ambazo zinapelekwa kwa ajili ya kusaidia wakulima zinaweza kukaguliwa.

Na. 477

Ujenzi wa Miundombinu ya Maji Taka Dodoma Mjini

MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE aliuliza:-

Wakazi wengi wa Mji wa Dodoma wamechimba makaro ya majitaka majumbani mwao, lakini kutokana na uchache wa magari ya kunyonya majitaka kwenye makaro hayo, husababisha kutapika majitaka hovyo mitaani jambo linalohatarisha afya za wakazi wa Mji wa Dodoma.

(a) Je, Serikali itakamilisha lini ujenzi wa mabomba makubwa ya majitaka yatakayunganisha mji wote ili kuimarisha usafi kwa Mji wa Dodoma?

(b) Je, ni lini Serikali itapunguza gherama za kuunganisha mabomba ya vyoo kwa mabomba ya majitaka machache ambayo tayari yapo?

(c) Je, ni lini Serikali itahamisha Bwawa la Majitaka la Swaswa lilioko Ipagala ambalo sasa liko katikati ya Kijiji na linatoa harufu mbaya na kali sana ambayo inaweza kuathiri afya za wakazi wa eneo hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. David Mallole, Mbunge wa Dodoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuboresha huduma ya majitaka katika Mji wa Dodoma awamu kwa awamu ili kutosheleza mahitaji ya Mji wote. Mwaka 2009, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Uswiss kuitia Shirika lake la Maendeleo (*SECO*), ilijenga mabomba ya majitaka yenye urefu wa kilometra 8.2 eneo la Hazina. Kuitia mradi huo, jumla ya Kaya 23 ziliunganishwa. Serikali pia kuitia program ya maendeleo ya sekta ya maji mwaka 2009 iliipatia Mamlaka ya Maji Safi na Majitaka Dodoma (*DUWASA*) gari la majitaka kwa ajili ya kuhudumia maeneo ambayo hayajafikiwa na mfumo.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali sasa ni kujenga mfumo mpya wa majitaka utakaotumiwa na Chuo Kikuu cha Dodoma na mfumo mdogo wa majitaka katika eneo la Makole. Jumla ya shilingi bilioni 6.8 zimetengwa kutekeleza kazi hizo na ujenzi utaanza mwaka wa fedha 2011/2012. Baada ya kukamilisha kazi hizo, huduma ya majitaka itakuwa imeboreshwa kufikia asilimia 37 kutoka asilimia 29 ya sasa. Serikali itaendelea kujenga mfumo wa Majitaka katika Mji wa Dodoma hadi huduma hiyo itakapowafikia wakazi wote.

(b) Mheshimiwa Spika, gharama za kuunganisha wateja kwenye mfumo wa majitaka katika Mji wa Dodoma ni Sh. 36,000/= kwa majumbani na Sh. 71,000/= kwa wafanyabiashara na taasisi. Gharama hizo zinahusisha upimaji, kuandaa michoro na kusimamia kazi. Hata hivyo, gharama hizo ni kidogo ikilinganishwa na gharama halisi na hazijabadiishwa toka mwaka 2002.

(c) Mheshimiwa Spika, *DUWASA* kwa kushirikiana na *CDA* imetenga eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 600,000 kwa ajili ya kujenga mabwawa ya kutibu majitaka. Usanifu ulikamilika ambapo mabwawa sita yatajengwa kwa awamu tatu, mawili kwa kila awamu. Jumla ya gharama za ujenzi ni shilingi bilioni 23 na mradi utatekelezwa katika awamu ya pili ya program ya maendeleo ya Sekta ya Maji itakayoanza Julai, 2012. Baada ya mradi huo kukamilika bwawa la majitaka la Swaswa halitatumika tena.

MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Naomba tu niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 1978 mpaka 1980 Serikali kwa kushirikiana na Kampuni ya *SABEJI Inter Plan* walitengeneza mifereji mizuri sana ya kupitisha maji ya mvua katikati ya Mji wa Dodoma. Kwa bahati mbaya mifereji hiyo, sasa mingine imeshajaa taka na mingine inapitisha maji machafu hasa ile inayozunguka eneo la Hospitali Kuu ya Mkoa na Soko Kuu la Majengo...

SPIKA: Mheshimiwa, ujue kwamba unauliza swali, sio hotuba.

MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE: Mheshimiwa Spika, sawa. Nilikuwa nataka tu kumwonyesha njia aweze kuona maji machafu yanapita wapi.

SPIKA: Muda hautoshi.

MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE: Mheshimiwa Spika, sasa napenda tu kujua Serikali ina utaratibu gani wa kuweza kuona kwamba, mifereji ile inabaki kuwa misafi ili kuweza kuimarisha usafi wa Mji wa Dodoma?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dokta David Mallole, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nimpongeze sana David Mallole, katika maswali ambayo tumekuwa tunapewa mara nyingi, yanayohusu huduma ya maji safi. Lakini Mheshimiwa Mallole, amezungumzia upande wa pili wa maji taka,kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Mallole.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kwa nini ile mifereji imekuwa na takataka na haisafishwi! Naomba niseme tu kwamba, kazi ya kusafisha mifereji ile ni kazi ya Serikali kuitia Manispaa ya Dodoma. Kwa hiyo, nawaagiza Manispaa ya Dodoma, wahakikishe wanasaafisha mifereji hiyo ili iwe safi. Ahsante.

MHE. IDD M. AZZAN: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa, tatizo la majitaka liliopo katika Manispaa ya Dodoma, linafanana kabisa na tatizo liliopo Dar es Salaam, na kwa kuwa bomba kubwa la majitaka linalopelea maji baharini, eneo la *Agakhan Hospital*, bomba lile linamwaga maji kando ya bahari na siyo katikati ya bahari, hivyo kusababisha harufu mbaya kwa wakazi wa eneo hilo, lakini na uchafuzi mkubwa wa bahari eneo la *Ocean Road* mpaka huku *Agakhan*, na watoto, vijana, wanakwenda kuogelea katika eno hilo...

SPIKA: Jamani, ni maswali, siyo hotuba.

MHE. IDD M. AZZAN: Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itaboresha miundombinu hiyo ya majitaka ili maji yasimwagike kando ya bahari?

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, naomba nichukue mapendekezo yake kwamba, tutahakikisha kwamba bomba lile ambalo limepasuka na linaleta harufu mbaya, tunalirekebisha ili lifanye kazi kama ilivyokuwa imekusudiwa.

Na. 478

Serikali Kuibua Miradi Mikubwa Kukuza Uchumi

MHE. MARTHA J. UMBULLA (k.n.y. MHE. CATHERINE V. MAGIGE) aliuliza:-

Moja ya mkakati uliotumika katika Mataifa ya Asia kukuza uchumi na kuondoa tatizo la ajira ni pamoja na kuibua miradi mikubwa ya maendeleo yenye kuajiri watu wengi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuibua miradi mikubwa kama vile ujenzi wa bomba la mafuta, uchimbaji mkubwa wa madini na makaa ya mawe na chuma ili kuleta maendeleo ya kiuchumi na kutoa ajira kwa vijana?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango wa Serikali wa kuibua miradi mikubwa kwa ajili ya kuleta maendeleo ya kiuchumi na ajira, Serikali imepitisha Sera mpya ya Madini ya mwaka 2009 na Sheria ya Madini ya mwaka 2010 zenye lengo la kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kijamii na kiuchumi.

Mfano, kuongeza na kuimarisha fungamanisho la Sekta ya Madini na sekta nyingine za kiuchumi. Kuboresha mazingira ya kiuchumi, kuvutia uwekezaji na kuongeza uwekezaji, ambavyo kwa pamoja matarajio ni kwamba, mikakati yote hii itaibua miradi mipy ya madini na sekta nyingine za nishati kuwaendeleza wachimbaji wadogo ili ushiriki wao uwe na tija kuhamasisha na kuwezesha uongezaji wa thamani madini nchini. Utekelezaji wa malengo haya utaongeza fursa za ajira nchini ikiwa ni pamoja na kuleta maendeleo ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeamua kujenga na kumiliki kwa asilimia mia moja bomba kuu litakalouganisha raslimali za gesi za *Mnazi Bay*, Songsongo, Kiliwani, Nyuni, Mkuranga, pamoja na gesi iliyogundiwa katika kina kirefu cha maji, *deep sea*, nje ya Mkoa wa Mtwara.

Ni matumaini ya Serikali kuwa kukamilika kwa utekelezaji wa mradi huu, kutoa fursa zaidi ya kutekeleza kwa miradi mbalimbali mingine ya maendeleo na kuvutia uwekezaji katika sekta mbalimbali zinazotarajiwa kutoa ajira kwa wananchi zinazohusiana na nishati hiyo katika shughuli za viwanda, uzalishaji wa umeme, viwanda vyta mbolea, mahoteli na taasisi nyingine za Serikali na za sekta binafsi. Aidha, Serikali kuitia taasisi zake ikiwemo *GST*, *STAMICO* na *National Development Cooperation – NDC*, inaendelea kuibua maeneo mengine ya uwekezaji yatakayoendelezwa ama na taasisi hizo au kwa kushirikiana na wawekezaji binafsi.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vijana wengi wanaoajiriwa kwenye machimbo hasa machimbo ya madini kama kule Mererani na kwingineko, huwa wanaajiriwa siyo kama ajira rasmi, bali huwa ni mapatano kati yao na wenye machimbo na hivyo kupewa ujira mdogo kwa kazi kubwa ambayo mara nyingi inahatarisha maisha yao.

Mheshimiwa Spika, je, Sheria inasema nini kuweza kuhakikisha kwamba, vijana wengi wanaoajiriwa kwenye machimbo wanapata malipo kulingana na kazi kubwa wanayoifanya? Sheria inawalinda ili wasiendelee kuhatarisha maisha yao?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Martha Umbulla kwamba, ni kweli ingekuwa vyema, siyo Mererani tu, lakini ambapo wale wachimbaji vijana wamepewa jina la Apolo, Mheshimiwa Ole-Sendeka analifahamu. Siyo kwa ajili ya Mererani tu, nadhani kwa uchimbaji wote mdogo. Ingekuwa ni vyema kwamba wale wenye leseni wanapofanya uchimbaji wao, vijana hawa wangekuwa na ajira zilizo rasmi.

Mheshimiwa Spika, lakini hilo limeonekana ni gumu kutekeleza kwa sababu ya namna ambavyo yale madini yenyewe yanavyopatikana. Yanapatikana kwa awamu, kwa msimu, kwa hiyo, inakuwa ni vigumu kidogo kutoa ajira ya moja kwa moja. Lakini nadhani hili linazungumzika, tutazungumza na wenzetu wa Wizara ya kazi, tulipokwenda Mererani tumelizungumza hili na umoja wao wale wa Apolo, tunalitafutia ufumbuzi wa kuangalia ni namna gani hili linaweza kupata utekelezaji.

MHE. HAMAD RASHID MOHAMED: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Sehemu kubwa ya ajira katika migodi iko kwenye ile kada ya juu, ile kada ya chini huwa wanapata ajira ndogo sana. Kwa mfano, ukichukua Afisa mmoja wa ngazi ya juu anaweza kuchukua Watanzania wasiopungua 1,000 wanaoajiriwa nchini. Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza sheria ya kwamba hawa wataalam wa juu wanahamisha utaalam kuwapelekea Watanzania na kulipwa mafao yanayostahili badala ya kupunjwa kama ilivyo hivi sasa?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sijui kama *ratio* ni moja kwa watu 1,000 baina ya kada ya juu na chini, lakini nadhani kwamba hili la kuhamisha utaalam, ili Watanzania wengi waweze kuajiriwa katika kada hizi. Hili ni jambo ambalo lilikuwa linafanyiwa kazi na linahimizwa na hata wawekezaji labda kule Barrick na wale wengine ambao walikusudia kuja, nimeona kwamba wameanza utaratibu wa kuajiri Watanzania wawili, watatu katika kada za juu. Mimi nadhani tatizo ni hii kada ya katikati ambayo huwa inajificha ambayo mara nyingi unakuta wataalamu wanaokuja ni kutoka nje. Mimi nadhani hapa tutajielekeza ili kwenye kada zote pawe na *proportionality* ya Watanzania kuwa wengi zaidi kama utaalamu na uwezekano na wingi wao unaruhusu.

Na. 479

Uchapishaji wa Noti Mpya

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI aliuliza:-

Benki Kuu ya Tanzania imeingiza katika soko, noti mpya ambazo zinatumika pamoja na zile za zamani, lakini kuna taarifa za kuwepo kwa wingi wa noti bandia kwenye soko jambo ambalo ni hatari kwa uchumi wetu:-

- (a) Je, ni sababu zipyi zilizofanya Benki Kuu ya Tanzania kuingiza noti mpya sokoni na zile za zamani zikiwemo?
- (b) Je, lini Serikali itachukua hatua ya kuwajibisha watumishi wa Benki Kuu ya Tanzania kwa kushindwa kudhibiti kuingia kwa noti bandia katika soko?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kawaida, Benki Kuu huchapisha noti zake nje ya nchi kwa mikataba na wachapishaji wanaopatikana kwa utaratibu unaozingatia Sheria za Manunuzi.

Mkataba baina ya Benki Kuu na mchapishaji wa noti za zamani zilizoko katika mzunguko ulimalizika mwaka 2008 na hivyo ilikuwa lazima kuanza kwa mchakato mpya wa upatikanaji wa noti nyingine. Kubadilisha toleo ni hatua ya kiusalama, hutoa nafasi ya kutumia teknolojia mpya na kupunguza gharama.

(b) Mheshimiwa Spika, tatizo la noti bandia kuingia katika mzunguko siyo la noti za Tanzania pekee bali linazisibu fedha za nchi zote duniani ikiwa ni pamoja na zile za nchi zilizoendelea.

Mheshimiwa Spika, tatizo la uhalifu wa kughushi noti linachangiwa kwa kiasi kikubwa na maendeleo ya kasi katika vifaa vya elektroniki vyenye uwezo mkubwa wa kunakili picha za rangi. Hata hivyo, naomba ielewewe kuwa kutengeneza noti bandia ni kosa la jinai chini ya sheria zetu.

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu inaendelea kutimiza wajibu wake chini ya sheria iliyoianzisha (*BoT Act 2006*) bila kukiuka na hivyo basi, hakuna sababu ya msingi ya kupelekea kuwachukulia hatua wafanyakazi wa Benki Kuu kwa jambo hili.

MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Mkataba wa Kuchapisha noti za zamani ulikwisha tangu mwaka 2008 kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, ni lini sasa Benki Kuu itaziondoa katika mzunguko noti hizi za zamani ili tubaki na aina moja ya noti?

Katika majibu yake Mheshimiwa Waziri amesema kwamba kughushiwa kwa noti kunachangiwa kwa kiasi kikubwa na maendeleo ya vifaa vya *electronic*. Lakini ninavyoolewa, kwa kiasi kikubwa, noti zinaghushiwa kutopteka na ubora wake hafifu. Je, Waziri anasema nini juu ya ubora hafifu wa noti mpya zilizoingizwa katika soko? Kwa kuwa zimekuwa zikichakaa upesi, zinachuja rangi na ni rahisi kuzigushi ukilinganisha na zamani.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA: Mheshimiwa Spika, la kwanza kuhusu ni lini noti za zamani zitaondolewa; noti za zamani ambazo zinazunguka na hizi mpya zimo katika kuondolewa na hivi sasa katika Hazina ya Benki Kuu, tayari noti za shilingi 10,000 na 5,000 karibu zimemaliza na zilizobakia ziko kwenye mzunguko. Noti zote zitapotea kitaalam baada ya kuzuiliwa na zitakuwa hazipo katika mzunguko kabisa. Kwa hiyo, hakuna muda katika pointi ambayo itakuwa haitumiki ili kuwarahisishia wananchi wasipate taabu za kwenda mabenki na kubadilisha.

Kuhusu ubora wa noti zilizopo na suala la kughushiwa, noti tulizonazo zina ubora wa kutosha na suala la kughushi kama nilivyosema mwanzo ni suala la kihalifu ambalo nalo linachukuliwa hatua. Jambo muhimu kughushi noti ni kuhakikisha kwamba zinawekwa *features* za kutosha za kiusalama ambazo ndizo zinazosaidia urahisi kutokuwa rahisi kuzighushi. Hili naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba noti zetu zina alama za kutosha, na pamoja na kughushiwa, kubwa ni elimu kwa watumiaji ili waweze kuzitambua zipi ni halali na zipi za kughushi.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda pia umekwisha. Sasa ninao wageni wachache kabisa hapa. Kwanza kabisa ninaye Mheshimiwa Said Elimamri, yeye sasa hivi ni Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya DAWASA, lakini pia ni *advocate* wa kujitegemea na maarufu sana, nafikiri mfano wa simba huyo, alikuwa kiongozi siku nydingi huyo, namkumbuka! (*Makofii*)

Tunao wageni wengine waliokuja kwa ajili ya mafunzo, hapa tuna wanafunzi 55 wa Shule ya Msingi Chalula na Mvumi Makuru Dodoma wasimame walipo, ahsante sana. Tuna wanafunzi wengine 55 wa Shule ya Msingi Jenerali Msuguri Dodoma, ahsante sana. Karibuni sana Walimu mjifunze vizuri mambo ya hapa. Tuna wanafunzi wengine 45 na Walimu wao wanenye kutoka Shule ya Sekondari ya *DCT Jubilee Dodoma*. Hawa na wenye wako wapi? Ahsante sana, karibuni na msome vizuri. Tuna wanafunzi 50 kutoka Shule ya Sekondari ya Nkhungu kutoka Dodoma, hawa wako *basement nadhani*, wamekosa nafasi watakuja baadaye.

Tunao wachezaji 30 wa mpira wa miguu kutoka Mkinga. Hawa ni kutoka Tanga. Aaah, kumbe ndio ninyi! Nilikuwa nashangaa, wanafunzi gani hawa wanatoka Jimbo la Mkinga? Nafikiri ni wageni wa Mheshimiwa Kitandula. Ahsante sana, karibuni sana tunawatachia michezo myema.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ni matangazo ya kazi. Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira - Mheshimiwa Daudi Lembeli, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo hii watakuwa na Mkutano saa 5.00 asubuhi katika ukumbi wa Pius Msekwa. Sijui kwa nini saa tano! Siyo kawaida yetu kukutana saa tano. Sikupata maelezo kwanini saa tano.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali - Mheshimiwa John Cheyo, naomba niwatangazie Wabunge kuwa kutakuwa na kikao cha Kamati leo saa tano katika ukumbi Na. 231. Hawa wamenieleza sababu zao. Nilipewa maelezo, kwa hiyo wameruhusisha kwenda.

Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini - Mheshimiwa January Makamba, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.15 mchana watakuwa na Mkutano katika chumba Na. 227.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji -Mheshimiwa Prof. Davidi H. Mwakyusa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 7.15 kutakuwa na kikao katika ukumbi wa Pius Msekwa 'B'.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Fedha na Uchumi - Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa 5.00 asubuhi watakuwa na kikao katika ukumbi wa Msekwa 'B'. Hawa wamenieleza sababu zao na nimewaruhusu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii - Mheshimiwa Jenista Mhagama, ameomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake ya Maendeleo ya Jamii kuwa kutakuwa na semina leo hii saa 7.30 katika ukumbi wa Pius Msekwa. Mtaonana huko huko maana naona kuna kugongana.

Katibu wa Wabunge wa CHADEMA – Mheshimiwa John Mnyika, anaomba niwatangazie Wabunge hao kwamba leo saa 7.15 mchana watakuwa na kikao katika ofisi ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani.

Katibu wa Wabunge wa CCM, Mheshimiwa Jenista anasema niwatangazie Wabunge wote wa CCM kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati ya Wabunge wote leo saa 7.15 mchana ukumbi wa Pius Msekwa. Mtajuana huko huko.

Yupo Mwenyekiti wa APNAC Tanzania – Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati tendaji ya APNAC, kuwa leo tarehe 23 huyu kutakuwa na kikao saa 7.15 mchana katika ukumbi wa Msekwa. Mnaona mlivyo wengi! Mnatakiwa *coordinate* na Afisa anayehusika na Kumbi, mtakutana pale, mtajua wenywewe. Yuko Afisa anayehusika na kumbi, kwa hiyo, kabla hamjaandika matangazo mnambawambia, mjue kama chumba hiki kitakuwa na shughuli au bado. Kwa hiyo, Katibu umebadilisha?

MHE. JENISTA J. MHAGAMA: Mheshimiwa Spika, hapana, samahani tangazo langu ni kwamba kikao chetu na Wawakilishi kutoka *UN* ni Wabunge Wanawake wote pamoja na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii.

SPIKA: Kile kikao alichotutangazia Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, kwa hiyo ni Wabunge Wanawake wote na Wajumbe wa Kamati yake. Basi, hiyo imeelewaka. Halafu ofisi inaniomba niwatangazie Wabunge wote kwamba Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi Serikalini (*GEPF*), unafanya maonyesho na usajili wa Wanachama wa Mpango wa Hiari wa Kujiveka Akiba ya Uzeeni. Hii shughuli itaanzia leo tarehe 23 mpaka 25 Agosti, 2011 katika viwanja vya Bunge. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote wanakaribisha kupata maelezo ya kina kuhusu Mfuko huo bila

kujali aina ya ajira zao. Kwa hiyo, kuna maelezo ya namna hiyo, *kwa hiyo* mkasilize yanaweza kuwafaa leo au kesho.

Waheshimiwa Wabunge, tunapoomba kuchangia, suala la kubadilishana na Mbunge mwininge ni sawa, lakini mmekubaliana huko kwamba mnabadilishana, lakini pia uwe na uhakika kama yule Mbunge atapata nafasi. Sasa unabadiilishana na Mbunge ambaye amechangia mara nne, mara tano, kwamba yeze ndiyo unabadiilishana, hiyo haiwezekani, kwa sababu vyovyote vile wewe usingepata nafasi. Kwa hiyo, nafasi yako inakuwa hakuna. Huwezi kubadilishana na Mbunge ambaye hata hawezu kufikiwa. Kwa hiyo, kuna wengine hapa ingawa wamebadilishana hawataitwa kwa sababu hawafikiwi, wale waliowapa nafasi hawafikiwi. Kwa hiyo, ni vizuri tukaendelea na utaratibu wetu.

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 68(7), wakati wa kipindi cha Maswali na Majibu, Waziri au Wizara ya Ujenzi ikijibu swali Na. 473, imelezea suala zima la watu wote wanaolipwa fidia katika ujenzi wa barabara ni wale ambaio barabara imewafuata. Lakini wale ambaio walijenga maeneo ya hifadhi ya barabara hawastahili kupewa fidia.

Mheshimiwa Spika, jambo hili limekuwa ni tatizo sugu la muda mrefu kwamba Serikali hii ni moja...

SPIKA: Tunaomba mwongozo wako.

MHE. DAVID Z. KAFULILA: Mwongozo wangu ni kwamba, Serikali hii ni moja, Wizara ya Nyumba na Makazi, kuititia taratibu zake inagawa viwanja mpaka maeneo ya hifadhi ya barabara. Wizara ya Ujenzi inakuja inabomoa nyumba za watu walizojenga maeneo ya hifadhi ya barabara kwa hoja ya kwamba wapo kwenye hifadhi ya barabara. Naomba mwongozo wako, majibu haya unaridhika nayo kwa misingi gani?

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, naomba ukae kwanza. Hiyo siyo mwongozo. Hii habari ya *contradiction* kati ya Wizara mbili, siyo mwongozo wa Spika. Naomba uliletu kwa utaratibu unaohusika. Naomba tukubaliane hivyo. Ni kitu wewe una-debate kwamba, kwanini viwanja vinagawiwa na kwa nini Wizara ya Ujenzi inasema bomoeni? Hili ni suala la mjadala, siyo mwongozo. Naomba tafadhili tuendeleee.

Waheshimiwa Wabunge, nilisahau kutangaza kwamba leo ni sikuu ya kuzaliwa Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, leo ni *birthday* yake. Kwa hiyo, ni mjukuu wangu, kwa sababu na mimi mjukuu wangu ana *birthday* leo. Kwa hiyo, tunaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012 - Wizara ya Maji

(Majadiliano yanaendelea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, wenzetu ambaio hawajachangia hata mara moja katika Wizara yoyote ni Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, Mheshimiwa Ester Midimu, hao ndiyo watakaoanza, watafutiwa na Mheshimiwa George Simbachawene waliochangia mara moja; Mheshimiwa Hamad Shabiby, Mheshimiwa Said Mtanda. Mheshimiwa Abuu, hayupo, na Mheshimiwa Ester Midimu naye hayupo.

WABUNGE FULANI: Yupo.

MHE. ESTER M. L. MIDIMU: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza kabisa, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri. Kwa vile mimi ni mara yangu kwanza kusimama katika Bunge lako Tukufu, napenda kuwapongeza akina mama wa Mkoa wa Simiyu kwa kunipa kura nyingi na mimi naahidi nitawatumikia vizuri. Pia napenda

kuipongeza familia yangu yote hususan kaka zangu, Ngassa na Malongo na kwa ushauri wao mzuri walinishauri vizuri katika kipindi cha kampeni, bila kumsahau Njalu Nagungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia kuhusu kero ya maji. Mkoa wa Simiyu una Wilaya tano; Bariadi, Meatu, Busega, na Maswa. Kuna Wilaya nyingine mpya ya Itirima ambayo bado hajaanza. Wilaya ya Bariadi kwa kweli wana tatizo kubwa la maji, wanawake wa Bariadi wanahangaika sana wanasumbuka sana na maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Bariadi, wanawake wanahangaika sana kwa kutafuta maji. Wilaya ya Bariadi, Kijiji cha Munze, Ng'wang'wali, Migato, Gangabilidi na Wadobana, wanawake wanahangaika sana. Kijiji cha Ng'wang'wali wana kisima kimoja kijiji kizima. Wanawake wanachota maji usiku, wanashindwa kuchota maji mchana kwa sababu ukienda kuchota maji asubuhi utatoka jioni kisimani. Wanatumia masaa sita kuchota maji. Mtu akienda saa mbili, anatoka saa sita. Kwa hiyo, wanawake wa Ng'wang'wali wameona ni bora wawe wanachota maji usiku saa mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukienda usiku kuchota maji, unakuta foleni kubwa. Hao ni wanawake wenzenetu, wanahangaika na watoto wadogo mgongoni usiku. Tunatakiwa tuwahurumie wananchi wa Simiyu. Bila maji nitakwenda kuwaambiaje mimi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wanawake wa Meatu wanahangaika sana. Tunatakiwa tuwahurumie, tuwapelekee maji. Maji wanachota usiku kiasi kwamba hata hawana raha na ndoa zao. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naongelea Wilaya ya Busega, Kijiji cha Ngasamo, Sanga, Bunga, Malili, Mwamigongwa, Imalamate, Nyangoko na Wang'engwe. Kijiji hiki cha Wang'engwe wanahangaika sana, naomba Mheshimiwa Waziri awahurumie wananchi wa Busega, hawana maji kabisa. (*Makofi*)

Nikija Wilaya ya Meatu, miradi ya maji inahitajika katika Vijiji vifuatavyo: Mwabusalu, Kisesa, Lingeka, Mwasengerera, Mwandu Itinde Jimbo la Mheshimiwa Mpina. Kwa kweli wanahangaika sana. Naomba wananchi wa Meatu wapelekewe maji, kwani nawahurumia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ifanye mpango Sekondari zote za Mkoa wa Simiyu wachimbe visima vya maji. Shule za Msingi zote pia wachimbe visima vya maji ili wananchi waweze kupata maji. (*Makofi*)

Vijiji vyote vilivyo kandokando vya Bariadi, Kisesa, Meatu na Tarime vichimbiwe malambo kwa ajili ya mifugo na binadamu, na kwa kuwa hivi sasa mito yote iko kwenye hifadhi, tunaomba basi tuwajali binadamu, tuijali na mifugo, tuchimbe mabwawa ya mifugo na tuchimbe visima vya maji ya kunywa, kwani wanawake vijijini wanahangaika na mimi nawahurumia wanawake wenzangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hata watoto wameathirika, shule wameshindwa kusoma, wanachota maji usiku kucha, asubuhi wanasinzia. Asubuhi maji hakuna, kwani maji Vijijini yanapatikana usiku.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Haya, hongera. Kwa Kiingereza tunaita ilikuwa *maiden speech*, maana yake hii ndiyo ya kwanza kabisa. Sasa nitamwita Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby na Mheshimiwa Saidi Mohamed Mtanda watafuatia.

MHE. SAIDI M. MTANDA: Mheshimiwa Spika, kwanza nitumie fursa hii kukushukuru na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nitumie fursa hii kumshukuru sana Ndugu yetu Mustafa Sabodo kwa utekelezaji wa mradi wa visima 700 vya maji. Namshukuru Sabodo kwa sababu maeneo mbalimbali ya Jimbo langu yamepata mradi huu kufuatia maombi ambayo Waheshimiwa Wabunge tulielekezwa hapa, tuombe kupitia Kamati ya Dkt. Msuya. Namshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, maeneo ya Jimbo la Mchinga, hususan Kijiji cha Matapwa na Mnyangala yamepata maji. Tunatoa shukurani zetu za dhati.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia wenzetu wa *Don Consult Ltd* kwa sababu wameweza kutuletea kisima pale Kijiji cha Namkongo. Kwa hiyo, tunaendelea kuunga mkono juhudzi zao kuhakikisha kwamba tatizo la maji katika Jimbo la Mchinga linapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, naishukuru tena Serikali kwa sababu katika kitabu hiki cha bajeti nilichokisoma Serikali imeahidi kutoa ushirikiano mkubwa kwa Halimashauri yetu ya Wilaya ya Lindi Vijiini ili kuhakikisha tatizo la maji katika Kijiji cha Milola na Mputwa inapatiwa ufumbuzi. Naishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bajeti, kwanza niseme bajeti hii ni finyu na nilivyopitia vitabu Wizara hii imeomba shilingi bilioni 446, lakini fedha zetu za ndani ni shilingi bilioni 41 pekee haiwezi kutosha haja ya kuleta mabadiliko makubwa katika Sekta ya Maji nchini kwa kuzingatia kuwa maji ni uhai kama ambavyo kauli mbiu ya Wizara hii inavyosema. Shilingi bilioni 41 fedha ambazo tuna hakika nazo, yaani fedha za ndani. Jana rafiki yangu Mheshimiwa Munde Tambwe alisema mradi mmoja tu wa maji pale Tabora unaghari muhimu shilingi bilioni 50, Serikali inatenga shilingi bilioni 41 ili kuweza kutatua tatizo la maji nchini. Hii ni ndoto, jambo hili halitawezekana.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya shilingi bilioni 387 ni fedha za nje na tuna uzoefu kwamba fedha za nje hazifiki kwa wakati, zinafika kwa kuchelewa. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba miradi hii iliyoinishwa katika bajeti ya Wizara ya Maji haiwezi kupata majibu katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, ukisoma dira ya Taifa, yaani *vision 2020 - 2025* kuna malengo matatu. Moja, ni utawala bora, uchumi imara na maisha bora. Lakini naamini kabisa, hatuwezi kufikia dira hiyo ya Taifa endapo maji vijiini yataendelea kuwa ni tatizo sugu. Waswahili wanasema sasa ni janga sugu la wazawa. Tatizo la maji sasa nchini limekuwa ni janga sugu, linalowaathiri wazawa hasa wa vijiini.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kwa sababu takwimu zinasema asilimia 70 ya dunia hii ni maji ingawa asilimia 2.5 tu ya maji hayo ni maji ambayo yanafaa kwa matumizi ya binadamu na mifugo, lakini sasa tunaona Serikali ikiwa hajielekezi kutatua tatizo la maji, hasa maeneo ya Vijiini. Hii inakera sana! Tunaiomba Serikali na tunaomba Watendaji na ukisoma hii bajeti, kuna usanii mwangi tu umepitia humu, miradi ya maji ya *World Bank* wanasema wametenga shilingi bilioni 86. Hivi Shilingi bilioni 86 utekeleza miradi mingapi ya maji? Miradi ambayo imekwama toka mwaka 2009 na leo tunaambiwa eti mwaka 2012 kuna awamu ya pili ya mradi wa maji wa *World Bank*, inafuata nini wakati hii ya kwanza hajatekelezwa? Jambo hili ni lazima tuliangalie kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nilikuwa napitia sera ya maji ya mwaka 1991 inasema, ifikapo mwaka 2002 wananchi wapate maji kwa umbali usiozidi mita 400. Ifikapo mwaka 2002 sera ya maji ya mwaka 1991 na bado tunaendelea na sera hii, mita 400, lakini pale Namkongo wananchi wanakwenda kilomita tano, pale Likwaya wananchi wanakwenda kilomita 10 kufuata maji, Kilolambwani hakuna maji, mita 400 iko wapi?

Mheshimiwa Spika, jambo hili linaudhi na mambo haya ndiyo yanayosababisha wananchi waichukie Serikali wanayoipenda ya Chama cha Mapinduzi. Hatuwezi kuvumilia. Watendaji wa Wizara hii ni lazima wajipange, wahakikishe hawamwangushi Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya M. Kikwete, lakini pia wasilitie doa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Toka mwaka 2009 mnasema mradi wa maji viji 10 mnaingia mikataba. Ni mikataba gani hii isiyo na maana? Mkataba gani

unasema tuchimbe kisima kwa miaka mitatu? Mwaka 2009 *Don Consult Lindi* anachimba visima, maji yamepatikana lakini hatufungi pampu, eti tunasema tunasubiri awamu ya pili. Awamu ya pili ya nini?

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine wanasma, Mheshimiwa Mbunge basi kama awamu ya pili ya kusambaza maji inachelewa, kwa nini Serikali isichukue hatua za dharura kufunga pampu kwenye *source* ili waweze ku-enjoy yale maji na baada ya hapo Serikali ikipata fedha, ndipo ianzu kusambaza katika maeneo mengine. Kwa nini hatusikii? *Quran* inasema: "wako watu wana macho lakini hawaoni na wengine wana masikio lakini hawasikii." Wizara hii haisikilizi kilio chetu. Wabunge wote toka jana wanapiga kelele hapa kuhusu *World Bank*, Serikali ichukue hatua za kunusuru miradi hii. (*Makofii*)

Wiki ya jana nilikuwa Lihimilo, wananchi wanasma, hakuna Mkutano kama hatuelezi kwa nini toka mwaka 2009 maji hakuna? Mkutano wa nini? Mnatuweka pabaya Waheshimiwa Wabunge na sisi ni vijana tunaotaka kukua na kuitumikia nchi hii, lakini kama Serikali hatatimiza wajibu wake, hatuvezi kufika huko na sisi hatuko tayari kama vijana. Leo ninasema kwa uchungu na sio tabia yangu hii. Lakini tatizo la maji vijiji ni tatizo sugu na pale Wizarani mnasema mnacho Kitengo cha Maji vijiji, kinafanya nini? Kununua magari ya kifahari na kutembea! Mnakagua miradi gani? Unakwenda pale Kiangala mradi wa maji, pampu imekufa, lakini hakuna anayejali, wananchi wanapata shida, mnasema *District Water Engineer*, wanafanya kazi gani?

Mheshimiwa Spika, leo nimeona niseme hili kwa sababu linaniumiza sana. Ukisoma llani ya Uchaguzi ukurasa wa 119 tunasema ifikapo mwaka 2015 tuhakikishe tumetoa maji kwa asilimia 75 Vijiji na asilimia 95 Mijini, itawezekana wapi kwa takwimu hizi?

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Lindi Vijiji ina takriban wakazi 275,000 lakini wananchi wanaopata maji ni 82,114 tu. Ni tatizo kubwa. Tuna vijiji 154, lakini vinavyopata maji ni Vijiji 98. Hivi unakwenda kwa wananchi kuwaeleza nini? Kwa nini Serikali haisikii kilio chetu? Kwa nini Serikali haiwasikilizi Wabunge wao? Maana wengine wanasma wana uwezo wa kununua magari ili wachimbe maji kwenye maeneo yao, lakini sisi ni Wabunge masikini, tumetumwa hapa, hatuna uwezo wa kununua magari kwenye fedha yetu ya mifukoni, na ndiyo maana tunasema kwa uchungu kwa sababu mwenye uwezo wa kutatua tatizo la maji ni Serikali peke yake kwa kushirikiana na mashirika mengine. Sisi Wabunge kazi yetu ni kusemea kero za wananchi hapa Bungeni. Wabunge wangapi wana uwezo wa kununua magari hapa?

MBUNGE FULANI: Hakuna!

MHE. SAIDI M. MTANDA: Mimi ni Mbunge awamu ya kwanza.

MHE. GEORGE G. SIMBACHEWENE: Suti zenyewe ndiyo tunanunua hapa!

MHE. SAIDI M. MTANDA: Suti yenyewe ndiyo tunanunua hapa, rafiki yangu Simbachawene ananiambia! (*Kicheko/Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pesa mliyonikopesha kwa ajili ya gari, nitakwendaje Jimboni vijiji 54 kule Kiwawa, Mputwa, Milola na Kilolambwani? Nitafikaje kama sina gari? Tunaiomba Serikali sasa isikie, na anayekwambia ukweli anakupenda, na sisi ni makada, nimekuwa Msaidizi wa Katibu Mkuu wa CCM miaka minne. Mimi ni Kada, nakipenda Chama change, lakini hatuko tayari kuvumilia kuona Watendaji wanaoiangusha Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Kila kukicha mtaalamu mwelekezi, upembuzi yakinifu, ni misamiati gani hiyo?

Mtaalamu mwelekezi mnamlipa shilingi milioni 900, mtaalamu mwelekezi anaelekeza nini? Mradi wa shilingi bilioni mbili, mnamlipa mtaalamu mwelekezi shilingi bilioni moja, mtaalamu mwelekezi, makaratasi ya uelekezi wake mnayaweka kwenye masanduku, hakuna maji Tabora, Mchinga, Lihimilo, Likwaya wala hakuna maji Kilolambwani, tutafika wapi?

MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI: Hata Mara.

MHE. SAIDI M. MTANDA: Mheshimiwa Kirigini ananiambia, hata Mara kule Mugumu Serengeti.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Hata Kisesa.

MHE. SAIDI M. MTANDA: Hata Kisesa kwa Mheshimiwa Mpina na Dkt. Titus Kamani yuko taabani kule, tatizo ni maji. Lakini pia yapo maeneo kwa mfano Miteja pale Kilwa, Mingumbi na Chumo kila siku Mbunge Murtaza Ally Mangungu anapiga kelele hapa! Tunaiomba Serikali sasa isikie kilio cha Waheshimiwa Wabunge. Hivi mta-*enjoy* nini kama Wabunge sisi hatutarudi tena hapa Bungeni? Mawaziri, Mzee Stephen Wassira atafurahi nini kama mimi sitakuwepo tena hapa? Siwezi kurudi humu kwa maneno tu, ni kwa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi kwa kupeleka maji Namkongo. Mnasema vijana wa CCM hawasemi, hatusemi! Tuna midomo na tuna uwezo wa kusema, lakini tunataka Watendaji wa Serikali watimize wajibu wao, ndiyo tunachokisema hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, huu mradi wa maji ukisoma ukurasa wa 53 Viji 10 imetengwa Shilingi bilioni 86. Waheshimiwa Wabunge wenzangu, mradi wa maji tayari kuna viji 126 ambavyo maji yamepatikana, lakini hayatumiki na mwaka huu wametenga Shilingi bilioni 86, uta-*supply* maji kwenye viji 126 ambavyo tayari maji yapo, lakini hayajasambazwa vijijini, inawezekana? Ndiyo maana nasema kuna usanii hapa. Wananchi wanaelewa, Watanzania wanaelewa na sisi Wabunge tunaelewa. Msitudharau kwa udogo wetu. Wananchi wametupa heshima kubwa.

Mkiangalia miradi hii, basi wale mnaojiita ma-*senior* mnagawanagawana tu, huu uende kwangu na huu uende kule na sisi *juniours* mnasema aah, huyu hata mwakani. Haikubaliki na wala haivumiliki! Tunaomba sasa Serikali ichukue hatua.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba wananchi wa Likwaya wanasema kwa kuwa tumepata maji, hao *World Bank* hawana fedha kwa sasa, kwa nini tusitoe maelekezo kwa Halmashauri zetu kwamba palepale tulipopata chanzo cha maji toka mwaka 2009 maji kisima kimechimbwa, wame-*flash* pale, kwa nini tusifunge hata *temporary pumps* kusubiri hizo fedha zenu za *World Bank*? Mzee Stephen Masatu Wassira, nihurumie mwenzio. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sitaunga mkono hoja hii mpaka kieleweke. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante na sasa nitamwita Mheshimiwa Mansoor Shanif Hiran na Mheshimiwa Nimrod Mkono na Mheshimiwa Susan Lyimo pia awe katika mstari.

Mheshimiwa Mansoor Hanif Hiran hayupo, sasa atafuatia Mheshimiwa Nimrod Mkono, naye hayupo! Ooh, yupo. Amevaa kofia inafanana na viti.

MHE. NIMROD E. MKONO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya pekee niweze kuchangia hoja hii muhimu sana Jimboni kwangu Musoma Vijijini. Awali ya yote, ningependa kukushukuru wewe na wenzangu walionitangulia, kwa maneno mazuri waliyoyasema kuhusu maji. Niliwahi kusema kwamba, mimi siungi mkono hoja hii kabisa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, siungi mkono hoja hii kwa sababu zifuatazo:-

Kwa miaka ipatayo kumi nimekuwa nakuja hapa, nazungumzia masuala makubwa mawili na imekuwa kama wimbo; moja ni kuhusu hali ya mazingira pale Buhemba. Huko nyuma aliyekuwa Waziri Mkuu, aliwahi kunitumia Mawaziri watatu kuja kuona hali halisi ya maji pale Buhemba. Mawaziri hawa alikuwemo ndugu yangu, Mheshimiwa Stephen Wasira, nadhani wakati huo akiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya, ambaye ni Waziri wa Maji, pamoja na Mheshimiwa Ibrahim Msabaha.

Vyanzo vya maji pale vimeharibiwa vyote kwa sababu ya uchimbaji haramu, *mercury* imejaa chini na hivyo Wananchi wa Buhemba hawawezi kunywa maji ambayo yana madhara. Ukiangalia kwenye bajeti hii, sioni fedha zozote zilizotengwa kwenda kudhibiti maradhi yaliyotokea, ambayo yanazidi kuendelea pale Buhemba kutokana na uchakavu wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, Watu wa Buhemba watanishangaa kweli kama nitaunga mkono Bajeti hii, ambayo haina chochote kuhusu maji Buhemba. Kwa kuwa mazingira ama vyanzo vimeharibiwa, kinachotakiwa ni kuchimba visima virefu kabisa visivyopungua kina cha mita mia mbili, uende *deeper* uhakikishe uchafu wa juu hauendi kule ndani. Bajeti hii ina upungufu mkubwa kabisa, kwa hiyo, siungi mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, la pili ni kwamba, hata kama bajeti ilikuwa inafaa, maji ya Buhemba yalikuwa yanatoka Butiama. Pale Kyarano, mgodi ulikuwa unatumia maji ambayo yamevutwa kutoka lambo la Kyarano. Huko nyuma kwa miaka kumi nilikuwa napiga kelele hapa nasema Watu wa Buhemba ni wahuni, hawatatufanya lolote, Serikali ilipuuza. Leo Meremeta imekimbia, imeacha matatizo makubwa ambayo sasa Serikali inawakabidhi watu wa STAMICO, eti wamefufuka na wanaweza kukidhi mahitaji ya Buhemba. Je, mmenipa nini? Pale Butiama tunakusudia kujenga chuo kikubwa pale tukitumia maji ya Kyarano ambayo yataavutwa kwenda Buhemba; shule hiyo itatumia nini? Hapo ndipo liliopo tatizo langu kubwa ninaloliona, kwa hiyo, siungi mkono hoja kabisa kwa hili na sioni kama kuna sababu au dalli yoyote ya kuwapoza watu wa Buhemba ama Butiama kuhusu maji.

Mheshimiwa Spika, jana nilifurahishwa sana na ndugu yangu, Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda, alipozungumzia Miradi ya Taifa ya Maji, ambayo imesahaulika kabisa. Moja kati ya Miradi hiyo ni *Trunk Route Four*, ambao ni Mradi wa Maji yanayotoka Mgango - Kyabakari – Butiama – Tiring’ati, halafu yanakwenda Rwamkoma – Bumangi, nadhani yalikuwa yanakusudiwa kwenda mpaka Buhemba. Mradi huu mkubwa wa Kitaifa uliobuniwa mwaka 1974 katika Awamu ya Kwanza, umesahaulika kabisa.

Pale Butiama, hivi sasa ndiyo nahangaika kutafuta maji ili watu wa pale wakidhi mahitaji. Mama Maria hana maji! Sitaki kuyasema hayo kila siku hapa, lakini maji hakuna. Kyabakari maji hakuna, Mradi wa Maji ya Mugango, Kiabakari, Butiama umekufa na ninaambiwa sasa ni miezi saba Wafanyakazi wa Maji pale Mgango hawajalipwa mshahara. Mradi mkubwa kama huo umesahaulika? Wale wafanyakazi hawajalipwa mshahara, kazi iliobaki ni kuchimba ile mifereji na kutoa mabomba kwenda kuyayeyusha yawe nondo ili wapate fedha.

Mheshimiwa Spika, hivi kweli Serikali ipo *serious* kwa haya mambo? Ndugu yangu Mheshimiwa Stephen Wasira, unajua ninavyolia, uko jirani pale, sina maji. Ukienda Kyagata kuna *trunk route* nyingine inatoka pale. Huko nyuma mwaka 2003, nilihangaika nikatoa fedha zangu mfukoni nikajenga tenki kubwa kwa shilingi zisizopungua nusu bilioni, nikakabidhi Mradi huo kwa Serikali, umetupwa na hata yule mlinzi aliuawa! Mradi wa Kyagata umekufa, Serikali imekuja na Mradi mwengine wa kisanii sanii pale Wegero. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, pale Wegero nitamsemea ndugu yangu Jaji Fredrick Werema, ambaye ni *Attorney General* wetu, pamoja na Dada Gaudentia Kabaka, wote wanatoka sehemu ya Wegero. Eti Serikali imejaribu kuchimba bwawa! Bwaha hili ni mojawapo ya yale mabwawa kumi niliyoahidiwa katika Halmashauri yangu ya Musoma. Tangu mwaka 2005 linachimbwa na wiki iliyopita nilondoka Bungeni kwenda kuhangainka kuona kama kweli hilo lambo lipo ama halipo! Nilipofika pale nikakuta mkondo tu wa ng’ombe, hakuna bwawa! Walichimba kidogo, maji yakaja yakavuta, yakinomba ule ukuta ambao ni wa udongo; kwa hiyo, kukawa hakuna bwawa.

Nilipowaita Wananchi na Waandishi wa Habari kuja kuona ujisadi uliotokea pale; mkandarasi amepewa fedha amekula, lambo halipo! Nimepiga kelele na Wananchi pale, kesho yake mkandarasi akanipigia simu na kuniambia kwamba, njoo tuongee; tuongee nini na yeye; tuongee ili nifunge mdomo! Mimi nimesema siongei na yeye nakuja kuongelea Bungeni. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya mkandarasi kusikia hivyo kesho yake mkandarasi huyo alipeleka Wegero magreda matano kuonesha yuko *site*. Hii ni Serikali kweli ama hakuna Serikali Musoma Vijijini? Hali kama hii itokee DC asijue; DED asijue; Mkuu wa Mkoa asijue; Afisa wa Maji asijue kwamba lambo la Wegero halipo? Siamenti lambo lilitapeliwa na mafisadi!

Mheshimiwa Spika, kuna mtandao mkubwa sana kuanzia huko juu Wizarani penyewe mpaka Halmashauri ya Musoma; fedha zikitoka huko juu zikija Musoma, wanadhani Musoma ndiyo

Manispaa ya Musoma na fedha za maji zinakwenda mjini, haziji kabisa Musoma. Ukiona hesabu za Halmashauri ya Musoma Mjini, hasa za maji ni za kuchekesha. *Accounts ziko qualified mwaka hadi mwaka, maji yanayopatikana pale ni yale yaliyotumia fedha zangu za Ubunge kwenda kuchimba visima pale Musoma.* Kwa hiyo, Serikali pale Musoma Vijijini imekufa, haipo! *A broken Government.*

Kwa miaka yote kumi niliyokuwa Mbunge pale, maji hakuna! Ukienda Mugango nasema hakuna, Kyabakari hakuna na pale kuna Jeshi, kuna Magereza na hawana maji. Ukienda sehemu za Majita, sehemu ya Muhoji, kuna bwawa pale kuna wfugaji wengi pale hawana maji, lakini wanasema Bugwema leo wanataka kumpa mwekezaji mwingine. Nasema siungi mkono hoja hii mpaka kieleweke, Buhemba mmefanya nini; Kyagata mmefanya nini; Muhoji mmefanya nini; *Trunk Route Four* mmefanya nini; Buswahili mmefanya nini na Butiama mmefanya nini! (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, huu ni usanii mkubwa kabisa; nitafanyaje Wananchi wangu wanalia maji hamna? Ukiangalia Mradi wa *Trunk Route Four*, leo ni karibu miaka 40 lakini hakuna kinachoendelea. Mradi umesahaaulika kabisa.

Mheshimiwa Spika, sina mengi, ndugu yangu Mheshimiwa Stephen Wasira, naomba sana unisaidie Wananchi wapate maji kwani maji ni uhai. Mwisho kabisa, nasema kuna *cluster schools* pale; kuna Oswald Mang'ombe, ambayo nillijenga mimi nikawapa Serikali kwa ahadi kwamba, watawapatia Wananchi wa pale maji. Hilo bwawa halijengwa mpaka leo, wanafunzi hawana maji, mimi nitaendelea kuwachimbia maji hadi lini? Kwa nini Bwala la Pale Chifu Ihunyo halina maji?

Niliambiwa kuna *quick wins*, barua zimeandikwa, kuna mtu pale anaitwa Sai katika Wizara ile, kila siku nikienda anacheka tu maji hakuna; najiuliza hivi anafanya nini pale Wizarani kwa nini wasimhamishe maana sisi kwetu Musoma Vijijini hana kazi kwetu, anashirikiana na mafisadi kuhakikisha fedha za maji hazifiki kule?

Leo badala ya kumwadhibu amebadilishwa kuwa Katibu; mimi nashangaa kweli; hivi tutafika tunakokwenda? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa huzuni kubwa, nasema siungi mkono hoja hii na pia nakusudia kutoa shilingi kwa Waziri ili ajue kwamba, hizi fedha hatazipata hata shilingi. Nadhani nikisema nitoe shilingi mbili ni halali, moja haitoshi kwa hasira niliyonayo. Kwa leo nasema ahsante sana, siungi mkono hoja. (*Makof!*)

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia hoja hii muhimu. Naamini wote tunakubaliana kwamba, maji ni uhai na kwamba, binadamu anahitaji mambo matatu tu ili aweze kuishi, nayo ni hewa, maji na chakula.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kunukuu maneno aliyyoyazungumza Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili, Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi, juzi tu wakati akitoa zawadi kwa wale watu waliokuwa na mashindano ya kusoma Korani Tukufu. Alisema hivi: "Nchi inatakiwa kuongozwa na Viongozi wanaofuata maadili ya dini. Viongozi wenyewe maadili ya dini wataongoza kwa kumwogopa Mungu na hawatafanya kama wajuavyo." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, ni wazi tumeona kwamba, katika mambo mengi ya nchi hii, Viongozi wanaongoza wanavyotaka na hasa tukizingatia katika Wizara ya Maji; hivi karibuni imetoka Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*), ikionesha ni jinsi gani Wizara ambayo naamini ndiyo imeshika uhai wa Wananchi wetu kwa sababu bila maji mtu hawezi kuishi; imefanya ubadhirifu wa zaidi ya shilingi bilioni sitini na tatu.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni la aibu sana na ninashangaa inakuwaje Mawaziri au Waziri aliyeuwepo bado anaendelea kuwa Waziri wa Wizara hii? Ni jambo la kusikitisha kuona zaidi ya shilingi bilioni 50 ambazo zimetengwa kwa ajili ya maji vijijini, lakini bado hakuna mtu hata mmoja ambaye amechukuliwa hatua! Ninaamini kuwa Serikali hii itaendelea kufanya uchunguzi ili wahusika waweze kuchukuliwa hatua, kwani kwa kweli wanafanya Wananchi wetu waendelee kupoteza maisha.

Mheshimiwa Spika, labda nitoe *facts* ambazo zinaonesha ni jinsi gani maji ni muhimu. Hivi ninavyoongea, kila mwaka zaidi ya watu milioni nne wanafariki kutokana na magonjwa yanayotokana na uchafu wa maji kwa kunywa maji machafu. Vilevile takwimu zinaonesha kwamba, katika dunia tunayoishi, muda wowote ule tukienda hospitalini nusu ya wagonjwa waliolazwa katika hospitali duniani kote ni watu ambao wameathirika na magonjwa yanayotokana na maji machafu, ikiwemo nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme kwamba, sitaunga mkono hoja hii hasa ikizingatiwa kwamba, mimi ni Kaimu Mwenyekiti wa Wanawake wa CHADEMA – Taifa na vilevile ni Makamu Mwenyekiti wa Wanawake Tanzania, kwa maana ya ulingo, Baraza au Jukwaa la Wanasiwa Wanawake Tanzania; na watanishangaa sana kama nitaunga mkono hoja hii wakati wanawake wamekuwa waathirika wakubwa sana wa maji hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba, akina mama wamekuwa wakitembea mwendo mrefu sana na ukiangalia takwimu zinaonesha wanaweza wakatumia saa saba mpaka kumi kwa siku wakienda kukinga maji na maji yenye wanayoyakinga wala siyo masafi. Kwa hiyo, unakuta kwamba, wanawake wanashindwa kufanya shughuli nyingine za uzalishaji kwa sababu tu ya kwenda kutafuta maji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwenda kutafuta maji, akina mama na watoto wa kike wanakutana na madhira mengi barabarani; wengi wamebakwa na wengine ndoa zimevnjika kutokana na matatizo ya maji. Jambo hili linasikitisha sana hasa ukizingatia kwamba, Tanzania ni nchi ambayo Mwenyezi Mungu, ametujalia vyanzo vingi sana vya maji. Tuna maji ya Maziwa, mfano Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa. Vilevile tuna mito mikubwa sana, lakini kinachosikitisha Wananchi hawapati maji. Pamoja na kwamba, wamesema asilimia 57 ya Watanzania wanapata maji, huu ni ule wastani wa jumla, lakini kwa kweli kuna maeneo ambayo asilimia tano tu ndio wanapata maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hakuna Mheshimiwa Mbunge mionganoni mwa Waheshimiwa Wabunge humu ndani, ambaye anaweza kusema kwamba, katika eneo lake wakazi wake wana maji ya kutosha. Kwa hiyo, nadhani ifike mahali kama tumeweza kuondoa kero ya barabara na mambo mengine, ni lazima sasa kero ya maji iondoke nchini. Tunaamini nchi yetu ina vyanzo vingi vya mapato na tunaamini kwamba, Serikali ikiamua Wananchi watapata maji. Kwa sababu kama kuna haya mabilioni ambayo yamepotea; ni lazima Serikali ina fedha za kutosha. Wananchi wanaweza wakapata maji safi na salama, bado tu hawaajaamua. Kwa hiyo, tunawaambia na tunaitaka Serikali ihakikisha kwamba, walau kwa mwaka huu, asilimia ya wanaopata maji iongezeke kutoka 50 ili ifike 80 ili baadaye mnapomaliza Awamu ya Nne basi Wananchi wote wawe wamepata maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, maji ni uhai na tunasema kwamba, bajeti hata ya Afya inakuwa kubwa kwa sababu tu ya kutibu wagonjwa ambao wanatokana na matatizo ya maji. Kwa hiyo, tunapotatua tatizo la maji, maana yake tunatatua tatizo la msingi la umaskini katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijielekeze katika eneo ninakotoka na eneo ninaloishi; ni jambo la kusikitisha kuona Moshi Vijiji eneo ambalo ninaamini lina vyanzo vingi vya maji, tunao Mlima Kilimanjaro, lakini wakazi wa maeneo ya Moshi Vijiji hususan Kata ya Mbokomu, Vijiji vya Korini Kusini, Tela, Rau, Mpirani, hawana maji kwa muda mrefu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimezaliwa katika maeneo hayo, kulikuwa hakuna shida ya maji mpaka miaka ya 1980, 1990, lakini sasa hivi hali imekuwa mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, ielewewe kwamba, wakazi wa maeneo ninayoyasema, tuna mila na desturi ya tunafuga mifugo ndani, kwa maana ya kwamba hatufugi nje kama wenzetu wanaotoka maeneo ya tambarare mfano, Wamasai, Wasukuma na kadhalika. Kwa maana hiyo, imekuwa ni tatizo kubwa sana kwamba, watu wanatumia maji hayo pamoja na wanyama na sasa hivi hatuna maji kabisa na hasa ikizingatiwa kwamba, maeneo mengi wanaishi wazee. Sote tunaelewa mzunguko wa fedha unavyokuwa mgumu vijiji, lakini vilevile maji yamekuwa ya

gharama kubwa sana, debe moja la lita 20 linauzwa mpaka shilingi 1,000; kwa hiyo, hili ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ukilinganisha mtu mwenye uwezo wa kuwa na bomba analipa bili labda ya shilingi 20,000 au 30,000 kwa mwezi wakati anayetumia maji ya madumu na mtu huyu ni maskini, anakuwa analipa zaidi ya mara kumi ya mtu mwenye uwezo. Kwanza, kwa siku mtu huyu anaweza akatumia hata shilingi 10,000, tukichukulia wastani wa familia ya watu watano na kila mtu anatumia ndoo mbili kwa siku, utakuta kwa mwezi mtu huyu anafikisha shilingi 300,000 wakati mtu mwenye maji ya kuvuta anatumia shilingi 15,000 mpaka 30,000. Kwa hiyo, hili ni tatizo kubwa sana.

Nilikuwa naomba watu wa vijiji ni waangaliwe kwa sababu wana matatizo makubwa sana ya kifedha. Vilevile pamoja na matatizo haya ya kifedha na umaskini wao, bado inawabidi wanunue maji kwa gharama kubwa na maji hayo unakuta wala siyo safi na salama, kwa hali hiyo watu hao wanaugua magonjwa mbalimbali.

Kwa hiyo, naomba kwa sababu nililiza swali mwezi Agosti tarehe 9, Mheshimiwa Naibu Waziri alinijibu na nataka nimwambie bado sikubaliani na majibu yake na nitaomba wakati anakuja kutoa majumuisho, atuambie ni lini Wananchi wa Moshi Vijiji katika Kata nilizozitaja na Vijiji nilivyovitaja, watapata maji ya uhakika. Nakumbuka mwaka 2008/09 tulikwenda na Mheshimiwa Naibu Waziri wakati huo Mheshimiwa Chiza, akaona vyanzo vya maji; cha ajabu siku hiyo maji yalitoka na baada ya hapo hakuna kilichoendelea. Kwa hiyo, inaonesha wazi wazi kwamba, tuna tatizo kubwa sana katika Wizara ya Maji na kama hakuna ufuatilaji wa karibu Wananchi wetu wataendelea kuumia.

Kwa hiyo, ninaomba wakati wa majumuisho Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, waniambie ni lini basi Wananchi hawa watapata maji ya uhakika ili waweze kuendesha shughuli zao za maendeleo na siyo kuwa wanatumia muda wao mwinge katika kukinga maji ambayo wala siyo safi na salama. Ninatambua kwamba, miaka ya nyuma tulikuwa na maji mazuri kabisa, safi, lakini jinsi tunavyoendelea, miaka 50 tunayosema tumethhubutu, tumeweza na tunasonga mbele, mimi nadhani kauli hiyo ni potofu kwa sababu hatujathhubutu na Wananchi wetu bado wanaendelea kuteseka. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nielekee kwenye Jimbo ninaloishi la Ubungo, Manispaa ya Kinondoni; ni jambo la kusikitisha sana kuona Jimbo la Ubungo, ambalo lina viwanda vingi na wakazi wengi kuliko Majimbo yote ya Dar es Salaam, bado jimbo hili lipo nyuma sana hususan katika suala la maji. Natambua kwamba, Mheshimiwa Mnyika amekuwa akitetea sana Jimbo la Ubungo, lakini bado matatizo yanaendelea. Jambo ambalo nataka kulizungumzia ni suala zima la Bwawa la Kidunda na maji ya Mto Ruvu Juu. Jambo hili limeongeleta sana, lakini kinachoshangaza, kumekuwa na kauli tofauti na kauli tata kutoka Serikalini. Inashangaza kuona katika randama ya Wizara wamesema kwamba, ujenzi wa Bwawa la Kidunda utamalizika mwaka 2013, lakini wakati Rais Kikwete alipotembelea Wizara ya Maji alisema hivyo hivyo kwamba, utakamilika 2013; na Mheshimiwa Waziri wa Maji katika Wiki ya Maji mwaka huu alisema hivyo hivyo, lakini sasa hivi ni jambo la kushangaza wanasesma kwamba litakamilika mwaka 2014. Sasa nilikuwa naomba kujua hizi kauli tata zinatokana na kitu gani, maana Waswahili wanasesma ukiweza kudanganya ujue pia na kukumbuka?

Sasa kwa kuwa wametoa kauli mbili tofauti, tunataka wakati wa majumuisho Waziri atuambie ni lini Bwawa hili la Kidunda litakamilika kwa sababu Wakazi wa Dar es Salaam wanategemea sana maji kutoka katika Bwawa hilo?

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nililotaka kulizungumzia ni suala zima la upotevu wa maji. Takwimu zinaonesha kwamba, Kimataifa upotevu wa maji unaweza ukawa ni asilimia 20, lakini kwa Jiji la Dar es Salaam peke yake, upotevu wa maji ni zaidi ya asilimia 50. Katika kipindi hicho, waliambiwa wapunguze walau ifike asilimia 40; mpaka sasa hivi katika Bajeti ya Wizara wamesema walau wamefikisha asilimia 48. Ina maana kwamba, kwa miaka miwili wameweza kupunguza kwa asilimia tano tu kwa sababu ilikuwa asilimia 53; je, itafikia lini asilimia 30 ili walau haya maji yanayopotea yaweze kuwafikia Wananchi?

Mheshimiwa Spika, ukitoka Kibamba ukaja Mbezi mpaka Kimara, upotevu wa maji ni mkubwa sana. Watu wameamua kuweka mabomba yao na wanaiza maji hayo na Serikali inaona. Nakumbuka Mheshimiwa Mnyika, aliuliza swali hapa Bungeni mwezi Aprili, 2011 na Waziri akasema angekwenda kufuatilia mpaka leo tunavyoongea si Waziri, si Naibu Waziri na wala hakuna Mtendaji ye yote wa Wizara ameweza kwenda! Hii inaashiria labda kuna *network* kati ya Watendaji pamoja na hao wanaiba maji; kwa sababu haiwezekani maji yawe hayapo, lakini kuna watu wanaiza wanaonekana. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani kuna mambo ya msingi ambayo Serikali inayaona lakini inashindwa kuyakemea na Wananchi wanaendelea kuteseka.

Mheshimiwa Spika, labda niseme tu; maeneo ya Jimbo la Ubungo ambayo yanapata tatizo kubwa la maji ni pamoja na Msakuzi, Mpigi Magohe, Manzese, Sinza Makabe, Goba, Mwamakuburi, Makoka, Kwembe, Msigwa na maeneo mengi. Sasa kama Kata hizi zote zina matatizo ya maji na hili ni Jiji la Dar es Salaam; ni aibu sana kuona akina mama, watoto, vijana, wamepanga foleni kuanzia asubuhi mpaka saa saba ndiyo wanakuja kupata maji katika Jiji la Dar es Salaam, ambapo wageti wengi wanapita wanaona Wananchi wapo barabarani na madumu ya maji. Kwa hiyo, pamoja na mipango mizuri ambayo ipo katika bajeti yao mwaka huu ni kwa kiasi gani wanatekeleza kwa sababu kila mwaka katika bajeti zao wanakuja na mipango mizuri lakini kila mwaka Wabunge wote wanakuwa wanasema hakuna maji katika vijiji vyao na katika Kata zao?

Jana Mheshimiwa Laizer alisema toka amezaliwa amekuta hakuna maji mpaka leo; naamini zaidi ya miaka 50 hakuna maji; sasa tutaendelea na utaratibu huu mpaka lini? Ninaomba sana Wizara iangalie na ihakikishe kwamba, ubadhifru ulioko ndani ya Wizara unakwisha ili Wananchi waweze kupata maji.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Moshi Kakoso, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla.

MHE. MOSHI S. KAKOSO: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kupata nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii.

Tatizo la maji ni kubwa sana katika Mkoa wa Rukwa hasa katika Wilaya ya Mpanda. Maji ni uhai, lakini Wananchi wa Wilaya ya Mpanda wanapata shida kubwa sana; huduma ya maji haipatikani mjini pale, yanayopatikana hayatoshelezi kwa familia ambazo zipo katika Wilaya ya Mpanda. Mbaya zaidi, hata madawa ya kutibu maji yale hayapatikani.

Mji wa Mpanda una vyanzo vikubwa vyta maji, lakini kumekuwa na tatizo la huduma hiyo. Mbaya zaidi, hata ule Mradi wa Vijiji Kumi haujaanza kutekelezwa ipasavyo. Vijiji Kumi vyta Mradi wa *World Bank* katika Jimbo langu tuna Vijiji vyta Karema, Ikola na Ngomalousambo, ambavyo bado huduma hiyo haujaanza kupatikana.

Je, ni tatizo lipi ambalo linaifanya huduma hiyo isipatikane wakati upembizi yakinifu ulishafanyika, lakini bado tuna matatizo makubwa sana na si kwa Jimbo la Mpanda Vijiji hata kwa Mheshimiwa Pinda kwenye Vijiji vyta Majimoto, Kibaoni, Mtakumbuka, Mwenge na Sungamilia, bado kuna matatizo makubwa sana ya huduma ya maji?

Mheshimiwa Spika, tatizo la maji kwa maeneo ya Mpanda ni kubwa sana. Wananchi wa Wilaya ya Mpanda Vijiji hawalali, wanatembea zaidi ya kilomita kumi kutafuta maji; jambo ambalo linawafanya Wananchi washindwe hata kufanya shughuli za maendeleo. Naiomba Serikali ilekeze nguvu kubwa katika maeneo ambayo kuna usumbufu mkubwa sana wa maji.

Tatizo la pili ambalo naiomba Serikali ilifanyie kazi kwa kina; kuna idadi kubwa sana ya wafugaji na mifugo. Mifugo hiyo imefanya vyanzo vyta maji viweze kupoteta. Kwa hiyo, tunapo jenga hoja ya kutafuta maji ni lazima tuandae mazingira ya kuchimba mabwawa yatakayokuwa yanasa idia kunywesha mifugo ili mifugo iache kuharibu vyanzo vyta maji.

Mheshimiwa Spika, tuna matatizo makubwa sana katika Kata ya Mpanda Ndogo, Mwese, Mishamo, Karema, Ikola, Kabungu na Kata ya Sibwesa, sehemu zote hizo zina uhaba mkubwa sana wa maji. Ninaomba sana Serikali iliangular hili; katika maeneo yetu kero kubwa zaidi ni maji; naishauri Serikali ni bora ipunguze hata barabara moja ikaelekezwa kwa ajili ya kutatua tatizo la maji. Kwani tatizo hili ni kubwa ambalo linajenga chuki dhidi ya Wananchi kuichukia Serikali. Tuna vijiji ambavyo havijawahi kupata hata huduma ya maji toka tupate Uhuru wa nchi hili; Vijiji hivyo ni vya Vikunge, Igagala, Kasekese, Kamusanga na Itunya, wana matatizo makubwa sana ya maji. Inashangaza sana Wananchi wanashereheke Miaka ya 50 ya Uhuru wa Taifa hili, lakini bado tuna matatizo ambayo yanawakera Wananchi kiasi kwamba, sasa wanakata tamaa na kuichukia Serikali yao. Ninaomba Serikali katika hili, waliangalie kwa kina ili waweze kushughulikia haraka matatizo ya maji ambayo yanaikabili Wilaya ya Mpanda.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba, Wilaya ya Mpanda imepeewa hadhi ya Mkoa Mpya wa Katavi, ambaao tayari tuna idadi kubwa sana ya watu na kunaanzishwa Wilaya Mpya ya Mlele, ambayo hakuna maandalizi yaliyofanyika ya miundombinu ya maji. Naamini katika kutekeleza haya, bado tunaleta tatizo kubwa la kusaidia Umma wa Wananchi. Naomba tunapofanya maandalizi ya Mkoa na tunapofanya maandalizi ya Wilaya, bado tuelekeze kuandaa miundombinu itakayowasaidia Wananchi kuweza kupata uhakika wa kupata maji. Tunalo tatizo la maji katika maeneo ya Kata ya Mishamo hasa kwenye Taasisi za Elimu na Taasisi za Afya.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Mishamo, Vijiji vya Isenga na Bulamata, kuna matatizo makubwa sana ya maji sambamba na Shule ya Sekondari ya Mishamo. Pia bado kuna maeneo ya Shule ya Sekondari ya Kabungu, Sekondari ya Mpanda Ndogo, Sekondari ya Katuma, Sekondari ya Mwese na Sekondari ya Ikola, maeneo haya wanafunzi wanapata shida kiasi kwamba wanashindwa hata kujisomea, muda mwingu wanapoteza kwa ajili ya kwenda kutafuta maji. Naiomba Serikali ieleteze nguvu zote kuhakikisha tunatatua tatizo hili. Mbaya zaidi na ambacho naijiliza; ni vigezo vipi vinavyotumika kuweka mgawanyo wa Mradi wa Vijiji Kumi?

Katika Jimbo langu, vijiji vitatu tu ndivyo vimewekwa katika mpango, lakini vijiji vingine vyote vimepelekwa katika Jimbo moja tu. Sasa nashangaa ni vigezo vipi na naomba Mheshimiwa Waziri atoe maelezo ya kutosha ili nielewe vigezo gani vinavyojengwa kuweza kupata hivyo vijiji vinavyoingizwa katika Mradi. Inashangaza sana, Wilaya ya Mpanda tuna vijiji 12 ambavyo vimepeewa Mradi huo, lakini kwenye Jimbo langu ni vijiji vitatu tu, Miradi mingine yote imepelekwa Jimbo la Katavi. Ninaomba nipewe maelezo ya kina, kwani Watanzania wote tunahitaji kuwa sawa na tunahitaji kupata huduma ilio sawa na haki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Visima Vifupi katika Vijiji vya Majalila, Illebula, Kasekese, Mnyagala, Kamsanga, Ifukutwa, Kabungu, Mantena na Igalula; kumekuwa na ujenzi wa kuchimba visima vifupi ambavyo kimsingi vinakwenda kama kisia. Visima vinachimbwa vinakuwa na futi kama kumi tu baadaye vinakauka na vinatumia fedha nyingi ambazo kwa kweli kimsingi ni kuwardhisha tu Wananchi wakati tunaipa hasara Serikali kwa kiwango kikubwa sana.

Kuna kisima ambacho kimechimbwa katika Shule ya Msingi ya Mpanda Ndogo, tena kwa mbwembwe nyingi, tafrija kubwa, kile kisima kilitoa maji kwa wiki moja mpaka ninavyozungumza leo hii hakitoi maji na visima vingi sana katika Jimbo langu ambavyo ni *design* kama hicho kilichopo katika Shule ya Msingi ya Mpanda Ndogo vipo katika Kijiji cha Ifukutwa na Mchakamchaka ambavyo havitoi maji. Kwa hiyo, kunakuwa na kitu ambacho wanakifanya wataalam wanachimba visima ambavyo ni vifupi sana na vinakuwa na gharama kubwa inayotolewa, lakini huduma ile haipatikani. Naomba Serikali waangalie na wafuatilie. Kama tutaendelea kupata tu taarifa za makaratasi bila kwenda kwenye hali halisi, kwa kweli tutakuwa tunawadanganya Wananchi na haki haitakuwa imetendeka kwa Wananchi wanaohitaji kupata huduma. Naiomba sana Serikali, waendelee kuchunguza Miradi inayosimamiwa hasa kule kwenye Halmashauri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, vyanzo vya maji ni muhimu sana; ninaishauri Serikali lazima ishirikiane na Wizara ya Mifugo ili kuhakikisha wanatenga maeneo ya kulisha mifugo na kuhakikisha wafugaji wanachimbiwa malambo ili kunusuru Wananchi na mifugo kutumia sehemu moja ya maji.

Tukichimba malambo, tutakuwa tumenusuru vyanzo ambavyo vinaharibiwa na mifugo; na lazima Serikali ichukue hatua za dharura kuhakikisha tunadhibiti kitu hicho; vinginevyo, vyanzo vyote nya maji vitakuwa vinatoweka kwa sababu ya idadi kubwa ya mifugo. Tunaomba hili lifanyiwe kazi kwa kina na lipewe uzito mkubwa sana ili kunusuru maisha ya Wananchi wengi wanaotegemea sana huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninaiomba Serikali iangalie kwa kina kwa kushirikiana kati ya Halmashauri ya Wilaya, Ofisi ya TAMISEMI na Idara ya Maji; Idara ya Maji imekuwa inasoma Miradi kwamba inakwenda kule chini, lakini hatua za utekelezaji zinakuwa za shida sana. Serikali yenye we hasa kupitia Wizara ya Maji, ni vizuri ikajishusha mpaka kule chini kuliko kuwaachia tu Halmashauri za Wilaya na ndiyo maana mnakaa mnadanganywa kwamba, tumetekeleza hiki wakati hakuna kilichofanyika. Ni vyema Idara, Wizara ikashirikiana na TAMISEMI kuhakikisha kile kilichoratibwa kinatekelezwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ni kuwaomba sasa Wizara ya Maji, mwakani mnapokuja kuomba bajeti yenu, mtenge fedha nyngi. Wizara hii ni muhimu sana, lakini bado bajeti inayotengewa ni kidogo mno, ndiyo maana kila Mheshimiwa atakayesimama hapa atapiga kelele.

Mheshimiwa Spika, nitaunga mkono hoja hii endapo nitapewa maeleo ya kina. Nashukuru sana. (*Makofî*)

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Awali ya yote naomba niweke kumbukumbu sahihi kwamba pengine miaka 50 ijayo inaweza ikatokea mjukuu wangu akaja kusoma *Hansard*, sasa ili mjukuu huyu akija kusoma *Hansard* asinione mimi mwedu au punguani, naomba niweke kumbukumbu sawa kabisa kwamba siungi mkono hoja hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, natokea Nzega Mji unaokua kwa kasi, mji ambaa una takribani wakazi wapatao laki tano, mji ambaa kwa asilimia kubwa wananchi wa pale ni wanachama ama wapenzi ama washabiki wa Chama Tawala, Chama cha Mapinduzi. Kwa heshima walionipa watu hawa naomba nieleze sababu kwa nini siko tayari kuonekana punguani mbele ya wajukuu zangu miaka 50 ijayo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu zifuatazo: Kwamba ni asilimia 37 tu ya Wananza ambaa wanapata maji safi na salama. Lakini zaidi ya asilimia 63 hawana maji. Sasa hawa asilimia 63 ambaa hawapati maji wanaishi vipi, wanapata wapi huduma ya maji, wanakunywa nini, wanapikia nini na wanajisafisha kwa kutumia kitu gani? Hii ni sababu mojawapo kubwa inayonifanya mimi kwa akili zangu timamu kabisa niseme kwamba siungi mkono bajeti ya Waziri wa Maji.

SPIKA: Mheshimiwa Kigwangalla samahani, nimemwona Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

WAZIRI, WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 64(1): Billa kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge.

Mheshimiwa Spika, Mbunge aliyesimama anasema kwamba, hataki baadaye mwanae amwone punguani au ana matatizo ya akili. Hayo maneno ana maana kwamba Wabunge wanaoiunga mkono hoja ni punguani au wana matatizo ya akili. Naomba hayo maneno ayaondoe. (*Makofî*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri nilivyomsikia ye ye anasema *Hansard* ambayo ye ye atakuwa ameonekana amechangia kwa kuunga mkono, kwa hiyo, hataki aonekane hivi alivyosema. Naomba aendeleee tu. (*Makofî*)

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Sababu nyingine inayonifanya nisiunge mkono hoja.

SPIKA: Endelea tu kujadili habari zingine, usijibu hapa.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA: Mheshimiwa Spika, mimi sipo huko. Sababu nyingine kubwa inayonifanya nisiunge mkono hoja hii ni ukweli kwamba sisi Wananzega tulipata matumaini makubwa sana pale ambapo Rais wetu Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete alipokuja Nzega kwenye kampeni na akatuahidi atatupatia maji safi na salama kutoka katika mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria. Lakini katika hali ya kusikitisha suala hili limekuwa linapigwa danadana, ukisoma katika hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri ambayo iliwasilishwa hapa jana Bungeni utaona amesema Oktoba mwaka 2011 watafanya *procurement* ya *consultant* ambaye atakuja kufanya upembuzi yakinifu sijui *detailed design* na vizungu vinatumika, mimi sielewi sana. Lakini sisi Wananzega tulitegemea mradi huu pengine ungekuwa ndiyo matumaini pekee kwa sisi kupata maji safi na salama haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika hali tu ya kawaida tunetegemea ahadi ya Mheshimiwa Rais iheshimike sana na ichukuliwe kama amri na kama agizo au dira ya utendaji kazi na viongozi wa Serikali lakini bahati mbaya sana ahadi hii kama vile inapigwa danadana na utekelezaji hauonekani kuwa *serious*. Tunaomba sasa Serikali itupe tamko hapa leo kabla sijaunga mkono hoja hii. Serikali itupe tamko kwamba ni lini watakamilisha hayo mambo mengine ambayo Mheshimiwa Mtanda aliyachangia vizuri sana hapa kabla yangu. Mambo sijui ya mtaalam elekezi, sijui mpembuzi yakinifu, sijui nini. Sisi Wananzega hatuelewi hayo. Sisi tunachohitaji tuone mabomba yameanza kuchimbiwa chini, tuone maji yameanza kutoka Nzega.

Mheshimiwa Spika, baada ya hilo, naomba nitupe lawama zangu moja kwa moja kwenye huu mradi wa maji wa Benki ya Dunia ambapo kwa bahati nzuri kwenye Jimbo letu la Nzega tuna viji viinne ambavyo vimepangwa kupata maji kutokana na mradi huu. Mpaka sasa wananchi wamechangia kwa kiasi kikubwa na sisi Wabunge wao tumewaunga mkono kwa kuchangia, kwa kweli tumejitahidi kutimiza wajibu wetu lakini katika hali ya kusikitisha mpaka ninavyoongea hapa ni viji viwili tu ndiyo maji yamepatikana na katika viji vingine vivili kati ya hivyo vinne hakuna uhakika wa maji. Kimojawapo ni kijiji cha Nkiniziwa ambapo kuna lambo la maji. Hili lambo ni la siku nyingi na lina maji mengi safi na salama na wananchi wamekuwa wakilitumia. Sasa naomba Serikali isikie kilio cha wananchi wa Nkiniziwa, pesa zao ambazo zilitakiwa ziletwe na *World Bank* badala ya kuchimba kisima ambacho kimeshindikana basi Wizara iongeze pesa kidogo, wafunge mitambo kwenye bwawa ili maji yaweze kusambazwa katika Kata ya Nkiniziwa.

Mheshimiwa Spika, lakini pale Kijiji cha Upungu ambacho kipo katika Kata ya Puge pia hakuna maji safi na salama na mradi huu ambao ulikuwa unaleta matumaini kwa wananchi wa Kijiji cha Upungu umeshindwa kutupatia maji na wananchi walishachanga. Leo hii mimi Mbunge nikienda kusimama pale kuongelea suala la maji nitaongea nini? Wamechanga pesa zao maji hayakupatikana na wao hawana maji. Mimi nitawaeleza nini watu hawa. Naomba sana Serikali ilitazame hili ili basi wananchi hawa pia waweze kupatiwa maji safi na salama. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na usanii mwangi sana unaoendelea kuhusiana na hili suala la mradi wa maji wa viji kumi kwenye Halmashauri na usanii huu umeanza tangu 2007, kila siku ni ahadi. Haya maji ya *World Bank* yatapatikana? Pengine nadhani tuwape muda Wizara watupe majibu ni lini tutapata maji ya uhakika angalau hivi viji kumi ambavyo wananchi wameshakuwa tayari kuchangia, wamechanga pesa na maji hayajapatikana mpaka leo hii. La sivyo, sioni haja kwa kweli ya kupitisha bajeti ya Wizara ya Maji kama hatuna mustakabali wa kupatiwa maji angalau katika viji hivi kumi ambavyo tumeahidiwa.

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine inayonifanya nisiunge mkono hoja hii ni kwamba, nilipita pale Butiama kwenye makazi ya Hayati Baba wa Taifa Mwl. Julius Kambarage Nyerere. Katika hali ya kusikitisha nilikuta maji pale hayatoki na katika kuongea na wale wahudumu wa pale niliambiwa maji yamekuwa hayatoki kwa takriban miezi saba mpaka leo hii. Ile familia ya Baba wa Taifa imekosa maji kwa muda wote huo, sishangai kama familia ya hayati Baba wa Taifa

inaweza kutelekezwa namna hii, familia ya akina Kigwangalla wasiojulikana watapata maji vipi? Hii inaonesha ni jinsi gani Serikali haiko *serious* katika kusambaza maji kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nigosie jambo ambalo wananchi wa Nzega wamenituma kusema na hili linahusiana moja kwa moja na ahadi za uwekezaji mkubwa wa uchimbaji wa dhahabu katika Jimbo la Nzega ambapo Mheshimiwa Dokta William Shija takribani miaka kumi na tano iliyopita wakati akija kuwatoa wananchi wa Nzega katika maeneo yao ambapo mgodi ungekuja kuwekwa baadaye alisema watapata maji, watapata ajira, watapata kila aina ya mambo mazuri mazuri ambayo yaliwawutia wananchi wale ku-vacate kutoka kwenye maeneo yao bila hata kulipwa fidia. Lakini leo hii miaka kumi na nne baadaye Dokta William Shija hayupo tena Wizara ya Nishati na Madini lakini wananchi wa Nzega hawajapatiwa maji, watu wa mgodi hawajachimba visima kama walivyoahidi na badala yake watu wa mgodi wa *Resolute* wanatumia maji takribani *cubic metres* kati ya 45,000 mpaka 60,000 kwa mwezi na hawalipii *bill* yoyote ile na hata kama wanadai kwamba wanalipia maana yake wanalipa kwa kiwango....

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante. Kengele ya pili hiyo. Samahani endelea hii ni kengele ya kwanza. Endelea Mheshimiwa Mbunge.

MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALA: Mheshimiwa Spika, nilitaka kuanguka hapa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba wananchi waliahidiwa kupewa maji safi na salama na watu wa mgodi. Kwa mradi huu ulikuwa na thamani ya billioni 1.5, watu wa mgodi wakaweka *water treatment plant* pale Nzega lakini hiyo *water treatment plant* ilifanya kazi kwa kipindi cha miezi sita tu na baada ya hapo ika-*cease ku-function* na toka waifunge mpaka leo hii ni trakriban miaka mitatu na maji hayawi *treated* pale Nzega.

Mheshimiwa Spika, wanaya-treat kienyeji kwa kumwagia dawa kwenye chanzo cha maji ambayo yanakuja kusambazwa mjini. Lakini pia walituhidi kututengenezea mtandao wa maji katika mji wetu mdogo wa Nzega. Lakini hayo hayajafanya na tunasikia mwakani wana mpango wa kuondoka. Sasa kama hii ndiyo hali ya utendaji wa Serikali yetu, nadhani wananchi wa Nzega wakae tayari sasa kwenda kufanya yale maandamano ambayo tuliamua kuyafanya, tulahirisha kwa nia njema tukitoa nafasi kwa Serikali kutekeleza ahadi zake, tukitoa nafasi kwa Serikali kuwabana watu wa mqodi ili waweze kutimiza ahadi zao.

Mheshimiwa Spika, kama hilo limeshindikana, naomba leo hii iingie katika kumbukumbu kwamba niko tayari kwa lolote, wananchi wa Nzega wamenituma niseme hivyo na wao wapo tayari kwa lolote na sisi sasa tutakwenda kuufunga ule mgodi sisi wenyewe kwa mikono yetu kwa sababu Serikali imeshindwa kufanya kazi yao, wameshindwa kuwabana wawekezaji na matokeo yake watu wa Nzega hawapati maji, watu wa vijijini waliahidiwa kuwekewa magati ya maji kule vijijini lakini hawapati maji, matokeo yake mifugo inakufa na wao wanachukua maji yetu kwa kiwango kikubwa namna hiyo wakati sisi wenyewe wanashindwa kutusambazia *cubic metre* laki saba kwa mwezi, wao wanatumia *cubic metre* 60,000 kwa mwezi. Hili halikubaliki na kama Watendaji na Mawaziri wanajiona wao wamekuwa ni *Prospero* wa kuhamasisha wizi na ubadhirifu na ku-control hatma ya wananchi wa Nzega. Leo hii kwa niaba ya wananchi wa Nzega nasema hatuvezi kukubali ghilba, hatuvezi kukubali dhuluma ambayo inahamasishwa na ma-*prospero* hawa wa uwekezaji. (Makoni)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba sasa *enough is enough* wananchi wa Nzega tutachukua hatua na tutachukua hatua kwa kuanza kwenda kuunganisha maji kutoka katika mabomba yanayopeleka maji migodini. Sisi wenyewe tutafungua kwa kutumia utaalim wetu, tutaunganisha mabomba pale, tutapeleka maji mjini badala ya kusubiri Serikali waifanye hiyo kazi, kwa sababu tumesubiri vya kutosha na Serikali imeshindwa hilo. Wanachimba maji katika kijiji cha Kabale ambapo wananchi wanakunywa maji ya tope, maji ambayo yanafanana rangi na *juice* ya *watermelon*, wakati wa kampeni niliona hii machozi yalinitoka. Mbunge wa Bukene yupo hapa ni shahidi yangu, Mkuu wa Wilaya ya Nzega ni shahidi yangu, maji mekundu yamejaa tope kama *juice* ya *watermelon*. Hali hii haikubaliki. Lakini hapohapo katika Kijiji cha Kabale na Uduu ndipo

kuna source kubwa ya maji ambayo watu wa mgodi wameweka visima vyao kumi na mbili halafu wanasema hawawezi kutugawia maji ambayo wanayachimba pale chini kwa sababu hayajawa *treated* wakati mji mzima wa Nzega unapata maji ambayo hayako *treated*. Sasa kwanini wanatwambia kwamba ni lazima maji yawe *treated*, wakati tayari watu wanakunywa maji ya tope, wanakunywa maji meupe kama maziwa? Wao wanasema tusubiri mpaka wa-*treat* maji ndiyo waweze kutupatia.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme leo hii tutapeleka wataalam wetu wenyewe, tutachangishana kidogo kidogo tulichonacho tutaleta na sisi hawa wapembuzi yakinifu watuungie maji wanakijiji wapate maji. Ni bora kunywa hayo maji yanayotoka mita 1000 chini kuliko kunywa maji ambayo yamejaa tope na yako juu. Kisayansi naona yale yaliyotoka chini zaidi yanakuwa salama, hayana *microbes* kuliko haya maji yaliyopo juu. Naomba Serikali watupe majibu ya hili na kama nilivyosema awali sioni sababu ya kuunga mkono hoja hii ya bajeti ya Wizara ya Maji kwa sababu hizo nilizozitaja.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. (*Makof*)

MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE: Mheshimiwa Spika, nichukue kwanza nafasi hii kukushukuru sana kwa dhati kabisa kwa kunipa nafasi ingawa ningependa ileweke si kwa upendeleo kwa sababu sijachangia mara nne, nimechangia mara mbili na nusu maana siku niliyochangia mara tatu nilichangia dakika kama saba hivi. Kwa hiyo, bila kuzungumzia maji usalama wangu huko Jimboni uko matatani na kwa hiyo kwa nafasi hii nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa kwanza niuelekeze kwenye miradi ya Benki ya Dunia. Neno Benki ya Dunia kwa maana ya miradi ya maji katika nchi yetu limekuwa ni kizungumkuti. Tumevumilia na wengine tumeingia humu kwa sababu tuliowaondoa kwa kesi za maji, lakini dalili inaonyesha na sisi tutaondoka kwa dhambi hiyo maana utekelezaji wake bado ni mgumu na dalili hazingoneshi kuzaa matunda ya hivi karibuni. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, miradi hii kumi ya kila Wilaya ilileta furaha kubwa na faraja kubwa kwa maendeleo ya watu wetu na hata mafanikio ya kisiasa ya mtu mmoja mmoja na hata kwa Chama chetu cha Mapinduzi. Lakini kama kuna kesi kubwa ambayo itatuletea matatizo kwa wote tuliofanikiwa kwa malengo ya kisiasa ni matatizo ya miradi ya *World Bank* na hata kinachosemwa sasa kwa hiyo miradi kumi na utekelezaji ambaa umefikia katika *levels* mbalimbali bado tujaribu kuwa wakweli na napenda Serikali ijaribu kuwa na ukweli wa wazi ili tuwe na lugha kesho na keshokutwa haitakuwa hukumu yetu. Sasa hivi uchimbaji wa visima umeanza, kule kwetu sisi tuna mtu anaitwa *O&A* ndiyo amechukua karibu Mkao wa Dodoma mzima na ye ye ndiye ana *drill* visima vyote vya Mkao mzima wa Dodoma. Aki-*drill* hapa amekuta maji hakukuta maji, anaondoka, anakwenda kijiji Kingine, aki-*drill* hapa amekuta maji, hajakuta maji, anaondoka.

Mheshimiwa Spika, kwa Jimbo langu niseme katika visima hivyo vitano ambavyo vimekuwa *drilled* na kubahatika kupata maji ni viwili. Sasa huko ambako amekosa na ameondoka sijui atarudi lini. Lakini hata hivyo vilivyokwishapata maji akishaondoka hatujui anayekuja, wanasema subirini awamu nyininge. Sasa mwananchi ameona maji yameshapanda, maji yanatoka halafu unamwambia mpaka wakati mwингine anapokuja mzunguko wa mtu mwингine ndiyo alete *pump*. Kwa kweli hiki ni kizungumkuti. Wenzetu wa *World Bank* pamoja na urasimu uliokuwepo katika miradi hii ya *World Bank* hakika sidhani kama Taifa wanatutende haki. Tunajua hatua ambazo Serikali imekuwa ikizifanya na jitihada ya Mheshimiwa Waziri wa Maji Mheshimiwa Mwandsosha katika kuhakikisha fedha hizi zinaingia lakini amechukua karibu miaka mitatu au minne kushughulikia tu kuingiza fedha kwenye *channel*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sasa utekelezaji na wenyewe ndio umeanza mambo mengine ambayo hata hatujui matarajio yake yatakuwa nini. Maana niwaambie tu watu wangu wale wa Uyenzele, Chinyanhuku, Kidenge, Makose na Kisima kwamba tungojee hiyo neema kama kweli itakuja, lakini ndiyo kilio changu hiki, natimiza wajibu wangu na sijui hali itakuwaje. Lakini, niwasemee Mheshimiwa Teu, mwenzangu ni Naibu Waziri hawezu kusema, wale wenzetu wa Kimagai, Chunyu, Iyoma, Mima, Mzase. Vile vile kwa Naibu Spika, Mheshimiwa Job Ndugai, kule Makawa, Njoge, Mlali, Mseta, Songambele, Mkoka, Chiwe, Ndalibo na Mlanje, kwamba, hatua

mbalimbali ambazo zimefikiwa, tuombe Mungu sana, lakini sidhani kama tutafikia malengo kwa sababu, sidhani kama kuna fedha ya kutosha kwa sababu miradi hii ina fedha nyingi. Lakini, tunavyosoma kwenye vitabu humu, sidhani kama kweli katika miradi kumi kila Wilaya, kama tutafika hata hiyo kumi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, si ajabu baada ya *ku-drill*, sasa watasema tuanze miwili au mitatu, hapo ndiyo mmetuletea sasa wenzenu humu ndani hatutarudi na kama kuna siasa inayokuja mwaka 2015 ni siasa ya maji. Siasa hii ya maji ni mbaya kwa sababu umeshindwa kuleta maji na umetua hidi kwa miaka mitano tuliyokupa umeshindwa, ondoka tunampa mtu mwingine na propaganda zimeanza sasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ubaya wa miradi ya *World Bank*, tayari ilishawakamua wananchi michango yao midogo midogo na ikawekwa kwenye akaunti ili kwamba zile asilimia tano... maana wengine asilimia tano, wengine hadi 10, kuchangia ili fedha za *World Bank* ziweze kutolewa. Kinachosemwa na wenzetu wanaotaka nafasi zetu, wanasema fedha hizo wamekula Wabunge wenu. Sasa hapo ndiyo nafasi itakapokuwa nyepesi kweli ya katuondoa kwa sababu tunaambwi sisi ndiyo tumekula zile pesa, maana kuzirudisha kule hatuwezi, kuhamisha mradi haiwezekani! Kwa hiyo, unabakia katikati, kwa namna yoyote utakavyosema, utaonekana wewe ni mwongo tu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli hapa hakika tunaomba Serikali iwe *serious* na jambo hili. Lakini, uko upande mwingine ambaao napenda niuzungumzie. Katika hili, ningependa nipayendekeze kwamba ni vizuri Serikali ikawa na Programu ya Kitaifa ya Maji inayotumia bajeti ya fedha zetu, siyo wafadhili. Maana ukianza kulalamika hapa unawalalamikia wafadhili, unaonekana kama hufikiri kwa busara kwa sababu unamlakamikia mtu anayekusaidia. Sina hakika kama hii ni *grant* au ni nini! Lakini, niseme tu kwamba ni vizuri tukawa na Programu yetu ya Maji ya Kitaifa ya miradi mikubwa mikubwa. Maana kwenye Halmashauri kule mnasema hawana uwezo wa kuweza ku-manage fedha milioni 500, milioni mia ngapi. Nadhani hii kwa kweli hata hivyo ndiyo imeleta mlolongo wa Mshauri sijui nini na nini.

Mheshimiwa Spika, wakati nipo Kamati ya *LAAC* niliwahi kwenda Wilaya ya Kiteto kule, nikaenda Kijiji kimoja kwa Mheshimiwa Nangoro, nikakuta kisima kimechimbwa, mashine zimefungwa, halafu kimetelekezwa kule, hakuna anayekwenda wala anayefuatilia. Sasa unajaribu kuona na wao wanasma sisi tumemaliza awamu yetu, tunamsubiri mwingine atakayekuja kuwashaa na *ku-pump*. Sasa, nasema watu wana shida ya maji, shida ya maji siyo *luxury*. Tunazungumzia habari ya umeme, umeme hapa siyo kitu. Watanzania wanauhitaji umeme, sawa, kwa ajili ya maendeleo ya viwanda. Lakini wanahitaji maji kwa ajili ya uhai. Kwa hiyo, maji ni muhimu zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia tuangalie miradi mingine ya maji ya mtiririko. Maji ya mtiririko ambapo mazingira yetu yalikuwa mazuri wakati ule, karibu kila Mkoa, karibu kila Wilaya na karibu kila maeneo katika nchi yetu walikuwa na miradi ya maji ya mtiririko. Miradi hii ilivyo sasa inakufa kwa sababu ni miradi iliyojengwa kuanzia miaka ya 1960 baada ya uhuru mpaka miaka ya 1975, ndiyo ilijengwa miradi mikubwa wakati ule. Miradi ile inakufa, mabomba yanachakaa na mabomba ya zamani yamekaa karibu miaka 40, lakini leo tunayonunua sisi mabomba yetu ukiweka pale, ni miezi sita, mwaka mmoja hakuna bomba tena. Hili nitalizungumza kwenye kipengele changu kinachofuata. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwaambie kwamba, ndugu zangu wale wa Lukole, Kingiti, Kibakwe, Chogola, Ikyuyu, Winza, Kikuyu, Pwaga, Chinyika, Seluka, Kidenge, Luhundwa na Vijiji vingine vyenye maji ya mtiririko, kwa sababu sisi kule Mpwapwa bado tunatunza sana mazingira, bado tunavyo vyanzo vya maji mtiririko yanayotoka milimani. Ingawa jitihada kubwa sana inahitajika katika utunzaji wa mazingira. Kwamba ni vizuri tukawa na programu pia ya kufufua, ya kukarabati hii miradi ya zamani, kuwe na programu maalum. Hii programu ya namna hii ndiyo mnaweza mkaziachia Halmashauri, ukiondoa ile programu ya Kitaifa ambayo itakuwa ina-deal/na miradi mikubwa mikubwa. Lakini hizi programu za namna hii ndiyo unaweza ukasema Halmashauri sasa watumie fedha zao wanazopata kwa ajili ya miradi hiyo ya maji.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie suala la vifaa vibovu vya maji (*mabomba, pumps, connectors na engines*) hapa ndipo kuna janga la Kitaifa. Kisima cha maji kilichojengwa mwaka 1975 mimi nikiwa bado mdogo, leo hii *pump* ile ile ya mkoloni inafanya kazi. Lakini *pump* ya leo ukiifunga pale, ni miezi sita, mwaka mmoja imejitahidi sana, hakuna! Sisi Mpwapwa pale tulichimba visima vifupi zaidi ya 150, kati ya visima vyote hivyo, hakuna kisima kinachofanya kazi sasa, vyote *pump* zake zimekufa. Hapa ndipo kuna janga kubwa na ningeomba Serikali ilione jambo hili. Vinginevyo hatutafikia malengo kwa sababu tutakuwa tunakwenda mbele, tunarudi nyuma, tunakwenda mbele, tunarudi nyuma. Vile visima vifupi tunavyovichimba, tunasema tumekwishamaliza tatizo, unakuta *pump* zake zikiwekwa zinakufa kesho yake.

Mheshimiwa Spika, nini kifanyike? Ni vizuri tukawa na *one center* au mtu mmoja anayetu-supply au nchi moja inayotu-supply vifaa hivi, kwa sababu miradi ya maji ukishajenga, watu wanataka kupanga mipango ya maendeleo, wanataka kutoka pale wasogee mbele, inakuwa vigumu kwa sababu tena unawarudisha kule kule, visima vile vinaharibika. Niwaombe sana Serikali, ni vizuri hii habari ya soko huria hii, hii habari ya kusema kila mmoja anaweza akaagiza kifaa, hebu Serikali irudi kwenye utaratibu wetu ule wa zamani wa kwamba Serikali ina standards zake na vifaa vyake vya kutoka nchi ambayo imeamua kwamba hawa ndiyo watatutengenezea pumps, hawa watatutengenezea mabomba. Sasa kuna mabomba siku hizi yanauzwa pale Dar es salaam, pale Kariakoo na viwanda vingine vya humu humu, mengine yanatoka nje, ukipiga teke, bomba linapasuka, kwa teke tu, bomba linapasuka! Sasa sijui wenzetu wa viwango wako wapi! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, juzi Jumapili nilikuwa kule Jimboni kwangu, nilikuwa nasimikwa kuwa Mzee wa Kanisa. Nilikuwa Chinyika kule, Kata ya Mlunduzi; Katika risala ile wameniambia mambo matatu:- Mheshimiwa, tunataka umeme, tunataka mnara, lakini na makufuri, yanayotengenezea sasa ni mabovu. Kufuri hizi za kufungia, lile la kufuri mimi pale sikulijibu, niliona kama jambo dogo. Lakini nilipokuwa narudi nipo kwenye gari natafakari, niliona ni jambo kubwa sana. Kama kuna security ya watu wetu, kama kuna security ya vile vibibi yetu kule nyumbani na nyumba zetu zisivyo imara, huwa ni vile vikufuri, ndiyo anaweka vihela vyake pale, anafunga na unakuta amevaa shingoni kafunguo kake, anaweka hapa. Lakini, wananiambia kufuri za sasa hivi sijui ni za namna gani, kwamba kila funguo inafungua kufuri la mwenzie. Kwa hiyo, nasema, haya mambo mengine madogo ndiyo yanayopelekea watu kutuchukia. Mtu unafikiri kufuri ikipita pale Bandarini jambo dogo, ni jambo kubwa. Mtu wa kawaida hawezikujenga nyumba akaweka mlango *strong*. Kwa hiyo, anachojuja kale kakufuri kake ndiyo katamsadia. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, pamoja na kusisitiza hili suala la mabomba na vifaa vya maji kwamba tuwe na *one stop center* na mtu tunaye-deal naye na nchi tunayoamua kwamba watuletee vifaa hivyo kwa mikataba na hao suppliers hata kama tunataka ku-deal na hizo sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni suala la utunzaji wa mazingira. Kama Taifa, kama kuna janga linalotaka kuikumba nchi hii ni uharibifu wa mazingira yetu na kuharibu vyanzo vya maji. Kila mmoja ajiulize wakati akiwa anakua, maji yaliyokuwa yanatiririka katika kile kijito cha karibu na nyumbani kwao, katika maeneo yao, katika mashamba yao, viko wapi? Vyote vimekauka. Tusipotunza mazingira, Serikali haiwezi ikafikia malengo. Haiwezekani kwa sababu kila ambapo uharibifu unazidi kuwa mkubwa, ndivyo ambavyo miradi inakuwa na gharama kubwa na sisi tuna tatizo la pesa, kwa hiyo utekelezaji wa miradi hiyo utakuwa ni mgumu. Tuhamasishe watu wetu watunze mazingira. Kilimo kwenye milima, kilimo kinachoendeshwa kwenye vyanzo vya maji kiwe ni marufuku, na Serikali ni vizuri ikawaambia. Wako Ma-DC wengine ni wavivu, DC kazi yake ni kulinda mazingira, upandaji miti. Makatibu Tarafa, Makatibu Kata, wafanye kazi hiyo, vinginevyo watu wetu wanamaliza na mkituachia sisi wanasiasa tunataka kura. Utakwenda pale watu wanafyeka, unasema bwana, ngojea uchaguzi upite, wanamaliza misitu. Kwa hiyo, wenzetu wafanye kazi yao vizuri, waokoe Taifa hili, vinginevyo tutaingia katika janga la kukosa maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na niunge mkono hoja maana nisipounga sasa haya mambo hayatafanyika. Naunga mkono ili hatua hii ambayo tunaifikiria iweze kufanyika na niwaombe Waheshimiwa Wabunge wengine, tusipounga mkono maana yake

hatuwapi pesa. Ingawa ni jambo la kinadharia sana, lakini ukweli umo. Kwa hiyo, tuunge mkono ili waanze hapa na tuwabane mwakani.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

TANZIA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 33(2) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, Spika anaweza kutoa taarifa wakati wowote.

Waheshimiwa Wabunge, jana tarehe 22 nilitoa taarifa kwenu kuwa Mheshimiwa Mussa Khamis Silima alipata ajali mbaya hapa Dodoma eneo la Nzuguni, ambapo mke wake Mwanakheri alifariki dunia hapo hapo. Aidha, nimewaarifu kuwa Mheshimiwa Silima na Dereva wake walipata majeraha makubwa na wamepelekwa Muhimbilli kwa matibabu zaidi. Leo, asubuhi hii, kabla ya kuanza Maswali, nimetoa taarifa kwenu kwamba nimeongea na Mheshimiwa Silima akiwa anaendelea kupata matibabu na kweli nimeongea naye.

Kwa masikitiko makubwa, naomba kuwatangazieni kuwa nimepokea taarifa kutoka kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuwa Mheshimiwa Mussa Khamis Silima amefariki dunia muda mfupi tu uliopita.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 149 ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, nitaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho Jumatano tarehe 24, saa tatu asubuhi. Kanuni hii inasomeka kama ifuatavyo:-

"Endapo Mbunge atafariki wakati Bunge likiwa katika shughuli zake, Spika ataahirisha shughuli za Bunge kwa siku hiyo kwa ajili ya maombolezo".

Aidha, naitisha sasa hivi Kikao cha Kamati ya Uongozi na Tume ya Bunge, tukutane ili tuweze kuangalia suala hili litaendeleaje baada ya hapo. Waheshimiwa Wabunge, naomba msimame tuweze kumkumbuka marehemu.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walismama kimya kwa dakika moja kumkumbuka Marehemu
Mheshimiwa Mussa Khamis Silima)*

SPIKA: Mwenyezi Mungu aipumzishe roho yake mahali pema peponi. Amina. Haya Waheshimiwa tukae. Bahati mbaya sana familia imepata matatizo makubwa sana. Hata ajali hii walipoipata walitoka kumzika kaka yake na Marehemu mke wake. Sasa katika muda wa siku tatu, amefariki kaka, amefariki mke wake na ye ye mwenyewe amefuata. Kwa hiyo, naahirisha Kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 5.57 Asubuhi Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatano,
Tarehe 24 Agosti, 2011 Saa Tatu Asubuhi)*